# Nipashe

Jumatatu Aprili 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580555

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

**Kaya** 10 zafikishwa kortini madai ya kutokuwa na vyoo

UKURASA 3



**Waziri** Mwambe aipa Benki ya CRDB siri ya uwekezaji

UKURASA 5



**Arteta amchimba mkwala Pepe**

UKURASA 20

# Viongozi wa dini wawajia juu wanasiasa wanafiki

• **Waahidi** kuwafanyia maombi maalum, Samia aonya wabunge wanaomlinganisha na Magufuli... *Ukurasa 2 & 3*



Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Baraza la Maskofu Katoliki (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga na Rais wa Zanzibar, Dk. Husein Mwinyi wakishiriki kuomba dua wakati wa Kongamano la Kitaifa la Viongozi wa Dini jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waziri Maji asimamisha watumishi

UK.2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**NANI KURITHI MIKOBA YA DK. BASHIRU CCM?**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kinatarajia kufanya Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa, Aprili 30, mwaka huu, ambao pamoja na...

UKURASA WA 9

**KESI 61 'UNGA' ZARIPOTIWA MKOA MMOJA KWA MIEZI 24**

JUMLA ya kesi 61 za dawa za kulevya zimeripotiwa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuanzia Januari 2019 hadi Disemba 2020...


UKURASA WA 10

**WANACHAMA SITA ACT - WAACHIWA HURU**

WANACHAMA sita wa Chama cha ACT-Wazalendo Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, waliodaiwa kuharibu mali za Ofisi ya Kata Mji Mdogo wa...

## Mafuriko yalivyokosesha makazi mamia ya kaya

UKURASA 8



Waziri wa Uwekezaji, Geoffrey Mwambe ,akipokelewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wa kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kushoto) alipowasili katika Semina ya uwekezaji jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU. Habari Uk. 5**

**MICHEZO** **MTIBWA YAHITAJI MAOMBI KUBAKI LIGI KUU** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

Waziri wa Uwekezaji, Geoffrey

# Waziri Aweso asimamisha watumishi 6 Maji

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAZIRI Maji, Jumaa Aweso, amewasimamisha kazi watumishi sita wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka hiyo, Mhandisi Tamimu Katakweba na Ofisa wa maji Bonde la Wami-Ruvu, Simon Ngonyani, kwa tuhuma za makosa mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya fedha na ofisi.

Uamuzi wa Waziri Aweso umefikiwa baada ya kutembelea ofisi za mamlaka hiyo mjini Morogoro wakati alipokutana na wafanyakazi baada ya kudai kupata barua ya malalamiko kutoka kwa baadhi yao, ikiwa ni muda mchache kukutana pia na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyokuwa na ziara kukagua vyanzo mbalimbali vya maji vya mamlaka hiyo na ripoti ya shughuli zinazofanywa.

Waziri Aweso alisema Mkurugezi wa MORUWASA alifanya kosa kwa kusaini mradi mkubwa wa maji unaojengwa kwa fedha za mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la nchini Ufaransa (ADC) ambao gharama yake ni Euro milioni 70 utakaokamilika mwaka 2021-2022.

Alisema walipata taarifa ya kusainiwa mkataba Aprili 14, 2021 bila wizara kuwa na taarifa na kumuelekeza Katibu Mkuu kufatilia suala hilo na mkataba huo usisainiwe hadi washiriki na kujiridhisha.

Hata hivyo, alisema kinyume na maelekezo, mkurugenzi huyo aliendelea na taratibu na kusaini mkataba huo kinyemela bila viongozi wakuu wa wizara kuwa na taarifa wala kushiriki na mwenyekiti wake wa bodi, mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya pia hawakuwa na taarifa.

Alidai pia kubaini mgogoro wa watumishi ulioundwa kikundi cha wafanyakazi waliohusika na ushawishi kwa wenzao, wakimpigia debe mmoja wa watumishi kupata nafasi fulani ya kiutendaji, dhidi ya ushindani wa wagombea wawili na licha ya mmoja kupata na mwingine kukosa watu hao walianza kumhujumu aliyepata nafasi kwa kushiriki vikao vya usiku kwenye hoteli na kwenda mbali zaidi kutaka kufanya mauaji.

Kuhusu kusimamishwa kwa ofisa mtedaji wa Bonde la Wami Ruvu, Ngonyani, alimtuhumu kutofanya kazi vizuri na wataalamu wake na matumizi mabaya ya fedha.

"Tunamsimamisha ili kupisha uchunguzi na uamuzi yote haya yanachukuliwa ili kuhakikisha malengo ya serikali kuhakikisha watumishi wanafanya kazi kwa weledi na maelekezo yanazingatiwa na si vinginevyo," alisema Waziri Aweso.

Aliwaonya watumishi wa wizara hiyo kujiepusha na ubadhirifu au matumizi mabaya ya chochote katika shughuli au miradi inayoendelea huku watumishi wa mamlaka za maji nchini na wa wizara wakitakiwa kushirikiana kufanya kazi kwa bidii na weledi kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), kuanza mara moja uchunguzi wa tuhuma zilizotolewa kwa watumishi hao ili kubaini kama kuna vitendo vyovyote vya ubadhirifu wa fedha na hatua zaidi ziweze kuchukuliwa.



Rais Samia Suluhu Hassan akielekea kuwatunuku Wahitimu wa Shahada ya Sayansi ya Kijeshi akiwa ameongozana na Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Profesa Eliamani Sedoyeka na Mkuu wa Chuo cha mafunzo ya Kijeshi Monduli Brigedia Jenerali Jackson Mwaseba katika viwanja vya Ikulu Chamwino mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. Shahada hizo zimetunukiwa kwa mara ya kwanza nchini na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Tanzania cha Monduli mkoani Arusha. **PICHA: IKULU**

# Viongozi wa dini wawajia juu wanasiasa wanafiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste, Peter Konki, amewaonya wanasiasa kuacha unafiki wa kujipendekeza kwa serikali iliyoko madarakani ili wateuliwe katika nafasi mbalimbali.

Askofu Konki, alitoa onyo hilo jana jijini Dodoma kwenye kongamano la viongozi wa dini lililofanyika katika ukumbi wa Chimwaga na kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hivi karibuni nimeona kwenye mitandao ya kijamii wanasiasa wanajipendekeza kwa kumsifia Rais Samia Suluhu Hassan na kutoa kashfa juu ya serikali ya Hayati Rais Magufuli, watu hawa wanajipendekeza ili waangaliwe kwenye nafasi, huo ni unafiki," alionya Askofu Konki.

Aliwataka Watanzania wasigawanywe na baadhi ya wanasiasa wanaomsifia Rais Samia na kumsema vibaya Hayati Rais Magufuli, huku akieleza kuwa hao wana ulafi wa madaraka na wanafanya hivyo kwa lengo la kuwagawa.

"Huu ni unafiki mbaya sana, wanafanya hivi kwa lengo la kutugawa, sisi tumetoka kwenye msiba hivi karibuni, lakini wanataka kuturudisha kwenye msiba tena. Niwaombe Watanzania tusijenge tabaka la udini, ukanda wala ukabila, na naomba nitoe wito kwa wanasiasa hawa wanaohubiri chuki waache mara moja," alitahadharisha Askofu Konki.

**ATAKA WAOMBEWE**

Kiongozi wa Shiha akitoa mada ya namna bora ya kumuenzi Rais Hayati Dk John Magufuli, Shekhe Azim Dewji, alitoa mfano wa shekhe aliyekwenda msikitini kuswalisha swala ya hadhuhuri (mchana) akiwa na farasi na alipoona hakuna mti wa kumfunga akapigilia msumari mrefu ardhini ili mtu akitaka kuswali afunge farasi wake, na pembeni kulikuwa na mtu anaona.

Alisema jioni alikuja shekhe mwingine kuswalisha akaona ule msumari na kuuliza nani kauweka pale kwa kuwa mtu anaweza kujikwaa na kuvunja kidole, akaung'oa huku mtu yule aliyemuona shekhe wa kwanza akiwapo.

"Walipomalizia kuswali mtu akaenda kwa shekhe wa mchana akamwambia shekhe kakutukana sana kuwa huna akili mana umepigilia msumari ardhini akang'oa akatupa...inatufundisha yule alikuwa na nia nzuri ya kumfunga farasi ili aswali na wa usiku alikuwa hajui msumari umewekwa kwa ajili gani aling'oa kwa nia nzuri, lakini wafitini huwa wanajaribu kufitinisha," alisema.

"Mama (Rais Samia) kila kitu kinategemea kwenye nia, rais aliyepita (Magufuli) alikuwa na nia yake, na wewe una nia yako wasikufitinishe wala wasikusumbue, hawa wakorofi tuachie sisi watu wa madhehebu tutawaombea na Mungu atawaangamiza kama alivyomwangamiza firauni.

**DK SHOO**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, akitoa mada ya kwanini kumshukuru Mungu, alisema kushukuru ni kukiri na kutambua kuwa yupo Mungu na yote yanayotokea kwa uweza wake na njia zao ziko juu ya uelewa wao.

"Mema au mabaya siyo ishara kwamba Mungu ametuacha, tunapaswa kushukuru kwa kila jambo, na kuelewa Mungu anataka kutufundisha nini, muhimu ni kuwa na unyenyekvu wa kusikiliza na kuelewa Mungu anataka kutufundisha nini."

"Ndugu zangu, Marais na nyinyi mliopewa madaraka katika nchini hii, wakati fulani nilikemea roho ya ukifutu, na ninaendelea kukemea, na tutaendelea kufanya hivyo, kwasababu ndiyo inayotupasa, tumshukuru Mungu ametoa viongozi wanyenyekevu na wanaomtanguliza Mungu katika mambo ya kuongoza," alisema na kuongeza:

"Chini ya uongozi wako (Rais Samia) Mungu ameshakuahidi, nasi tumeona wanasema nyota njema huonekana asubuhi nasi tumeshaona, chini ya uongozi wako kuna ahadi za Mungu," alisema.

**ASKOFU CHEYO**

Askofu wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi, Alinikisa Cheyo, alisema ni wajibu wa wananchi kuombea viongozi ili kuwapa hekima na maarifa ya kuongoza nchi.

"Tuwaombee viongozi wa ngazi zote kwa umoja wetu, Biblia inasema mamlaka zote zinatoka kwa Mungu na hakuna anayetoka kwa shetani, huwezi kumchukia mtu unayemuombea hivyo tuwaombee viongozi wetu baraka," alisema.

**MUFTI ZUBERY**

Naye Mufti Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubery, alisema katika alama zinazomfanya mtu aonekane ana dini ni kuipenda nchi yake.

"Tunafundishwa kuwa wazalendo na tuipende nchi yetu, maana Hayati Magufuli ametuachia mafunzo likiwamo la utu, alikuwa akiwajali watu na kuwasaidia wanyonge kupata haki zao. "Alikuwa na ukarimu kwa watu, lakini kubwa sana ni kujishusha maana ni silaha kubwa sana kwa viongozi na alikuwa akifanya hivyo enzi za uongozi wake," alisema Mufti Zuberi.

Alisema pia Hayati Magufuli, alikuwa akitatua matatizo ya watu yaliyokosa suluhu, alijenga nidhamu maana kuna watu walikuwa na kesi ya uhujumu uchumi, lakini alipambana nao.

Alisema Magufuli, alijenga heshima na hata alipokuwa akienda kwenye nchi za wengine walikuwa wakisikia jina lake wanawahudumia haraka na waliowaomba wamwazime Rais Magufuli.

"Pia alikuwa na ujasiri na uthubutu wa kufanya mambo makubwa kwa maslahi ya umma, alijenga uadilifu na uaminifu kwa watumishi wa umma, watu wanahudumiwa kwa wakati tofauti na ilivyokuwa zamani," alisema.

Mufti alisema Hayati Magufuli alikuwa akijali viongozi wa dini hadi wakajisikia raha na kupata imani kuwa kumbe wana wajibu wa kuisaidia serikali.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe, Salehe Omari Kaabi, akitoa mada ya utii na uzalendo, alisema ni muhimu Watanzania kumtii Mungu ikiwamo viongozi waliopewa mamlaka, kuacha mabaya, yenye hasara aliyoyaonya Mungu.

HABARI KITAIFA

# Samia: Acheni kunilinganisha na Hayati Magufuli

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujikita kwenye mjadala wa bajeti na kuacha kutumia muda mwingi kumfananisha yeye na mtangulizi wake Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dodoma, wakati akitoa hotuba yake kwenye Kongamano la Viongozi wa dini kitaifa.

Alisema kuwa amekuwa akifuatilia kwa muda kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni na kuona jinsi wabunge wanavyobisha katika ajenda ambazo hazina afya kwa taifa.

"Inasikitisha watu wanapiga ngoma kwenye mitandao ya kijamii kunifanisha na Magufuli na bungeni watu wanacheza hasa ngoma hiyo, hili jambo halina afya kwa taifa kwani Samia na Magufuli ni kitu kimoja," alisema. Alisema kuwa hivi sasa ni kipindi cha Bunge la Bajeti, wabunge wanatakiwa kujikita kujadili bajeti yenye maslahi na wananchi na kuacha na ajenda ambazo hazina afya kwa taifa.

"Niwaombe wabunge mfanye kazi kama ambavyo Bunge linatakiwa kufanya siyo kuleta ajenda ambazo hazina afya kwa taifa za kulinganisha mimi na Magufuli," alisema.

Alisema pia watu wanashindwa kuelewa kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya awamu ya sita na ile ya tano kwa kuwa yeye anatokana na awamu hiyo.

"Mimi awamu hii imengia madarakani bila kupigiwa kura na kiongozi ni kutoka chama kilekile hivyo hakuna tofauti yoyote mambo ni yaleyale," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kuwa katika awamu ya sita watahakikisha wanaendelea kusimamia suala la nidhamu ya kazi pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi.

Alisema pia wataboresha mazingira ya ufanyaji biashara pamoja na kuvutia mitaji kutoka nje ikiwa ni pamoja na kukuza mahusiano ya kimataifa.

"Serikali hii itaendeleza mema yote yaliyofanywa na Rais Hayati Magufuli na kuanzisha mema mengine katika awamu hii ya sita," alisema.Akizungumzia suala la ugonjwa wa Corona alisema ameshamaliza kuunda kamati ambayo itashirikiana na Wizara ya Afya kuona njia ambayo taifa itatumia ili kulinda nguvu kazi yake.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa dini nchini kuendelea kuelimisha waumini wao juu ya kuchukua tahadhari zote dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Vile vile, aliwataka viongozi hao kutoa elimu kwa wananchi kuachana na wizi, ufisadi ubadhirifu pamoja na uzandiki.

"Hapa lazima nipigie mstari kuna uzandiki mkubwa sana hasa katika mitandao ya kijamii mtu anaweza kuzusha lake na kutaka kuaminisha watu, hivyo waombeni na sisi tutaendelea kwa kushughulikia pia kwa namna yetu," alisema.

Alisema wakati huu ni muda wa Watanzania wote kuzika tofauti zao na kuwa wamoja ili kila mmoja kushiriki katika kulilietea maendeleo taifa na kuacha, ubaguzi, ukabila, udini na itikadi.

**MTOTO WA MAGUFULI**

Akitoa neno kutoka familia ya Hayati Magufuli, Joseph Magufuli, aliwashukuru Watanzania na viongozi kwa kuwafariji.

"Mama anawashukuru sana kwa kuliombea taifa baada ya kumpoteza Rais, kilikuwa ni kipindi kigumu, mama ameshindwa kuja kwasababu yupo kwenye matibabu alipata mshtuko kutokana na msiba wa baba," alisema.



Wahitimu wa Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (Bachelor Degree in Military Science - BMS) wakiwa tayari kutunukiwa shahada zao na Rais, Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, katika viwanja vya Ikulu Chamwino mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. Shahada hizo zimetunukiwa kwa mara ya kwanza nchini na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Tanzania Military Academy - TMA) cha Monduli mkoani Arusha, ambapo wahitimu hao pia walitunukiwa Kamisheni na Rais hapo hapo uwanjani. **PICHA: IKULU**

# Wapelekwa kortini kisa makazi yao kukosa vyoo

**Na Steven William,** PANGANI

WATU 10 wamefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo wilayani Pangani mkoani Tanga kwa kosa la nyumba zao wanazoishi kutokuwa na vyoo. Hayo yalisemwa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kimang'a wilayani Pangani, Alfani Rashii, wakati akimueleza Katibu wa CCM wa wilaya hiyo na viongozi wengine wa chama tawala walipofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi katika kijiji hicho. Rashidi alisema walifanya msako wa kutunza mazingira katika kijiji hicho na kukuta nyumba kumi hazina vyoo, hivyo waliwapeleka mahakamani.

Alisema waliwakamata watu hao kwa kosa la kukosa vyoo kisha kuwapeleka katika baraza la kata kupigwa faini ama kupelekwa mahakamani. Alisema serikali imeagiza kila mwananchi atunze mazingira sehemu anayoishi, lakini baadhi ya wananchi wa kijiji hicho hawataki kuchimba vyoo. Katibu wa CCM Wilaya ya Pangani, Mohamed Moyo, alisema viongozi wa kata,vijiji na diwani kila mtu ajue wajibu wake wa kufanya kazi ili kuwaletea maendeleo wananchi pamoja na kusikiliza kero zao na kutatua migogoro.


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**KatikaMahakamayamwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamiziwamirathi NO.111/2021**

**Ombi la SHARIFU BAKARI SEIF Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu BAKARI SEIF YUWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 18/05/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe16/04/2021

Tarehe 16/4/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO



FSSP Field Support Services Project | Tanzania
pwc Canada

**CONSULTANCY POSITION FOR FSSP RESULT BASED MANAGEMNET (RBM) SPECIALIST**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy Services as a **Results-Based Management (RBM) Specialist** to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The **RBM Specialist** will provide technical support and advice to Global Affairs Canada through use of an accompaniment model for on-the-job coaching/participatory training on RBM with DFATD project implementing partners and potential partners, to ensure that projects are implemented and reported on effectively.

Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:

i. Master's degree in relevant discipline from a recognized University.
ii. Five (5) years of professional work experience in the international development sector, particularly with Tanzanian project implementing partners
iii. Five (5) years professional work experience designing and delivering capacity building workshops in project design, RBM and reporting
iv. Five (5) years professional work experience developing project logic models and performance management frameworks using participatory approach with complex stakeholder groups.
v. Experience integrating elements of gender equality change and results measurement into complex monitoring and evaluation systems, including constructing and measuring gender equality results statements and analysing gender equality results data against a gender-specific or gender-integrated performance measurement framework.
vi. Experience working with stakeholders from Non-Government Organizations and Government.

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

- Data management skills (collection, cleaning, analysis, interpretation and presentation), documentation of lessons learnt and impact stories;
- Risk management skills (identification, analysis, responses planning and monitoring);
- Strong report writing and oral and visual presentation skills;
- Advanced professional proficiency in spoken and written English – level 4 and Kwahili – level 4 as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng**; and
- Knowledge of gender equality and equity policy priorities and processes in Tanzania.

Interested candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org**. Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **02 May 2021 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

# Kunenge akerwa ubabaishaji miradi ya maendeleo

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, amesema hataki kuona ubabaishaji katika utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo inayofanyika ndani ya mkoa huo huku akiwataka wasimamizi kuikamilisha kwa wakati.

Aliyasema hayo jana wakati alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua miradi minne ya kimkakati inayohusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara inayoendelea katika maeneo tofauti ndani ya mkoa huo.

Pia, Kunenge alimuagiza mkandarasi kutoka kampuni ya JASCO anayesimamia ujenzi wa barabara ya Makongo kukamilika kabla ya mwezi Oktoba ili iondoe adha inayo wakabili wananchi wa eneo hilo.

Alisema mradi huo unapita katika baadhi ya maeneo ambayo kuna miundombinu ya maji na umeme na taasisi husika zishirikiane na mkandarasi huyo ili kuihamisha na kupisha ujenzi huo.

"DAWASA na TANESCO) mkafanye kazi kwa kushirikiana na mkandarasi huyu ili kuondoa miundombinu ya maji na umeme iliyopita kwenye mradi ili asije akapata kisingizio chochote cha kuchelewesha kazi hii," alisema.

Alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 4.5 imegharimu zaidi ya Sh. billion 8.2 na ni moja ya njia muhimu zitakazosaidia kutatua changamoto ya foleni katika Barabara ya Bagamoyo.

Pia, alikagua ujenzi wa barabara ya Madale kuelekea Wazo yenye urefu wa Kilomita sita ambayo imegharimu zaidi ya Sh. billion 9.7 inayosimamiwa na mkandarasi kutoka kampuni ya MECCO.

Kungene alimtaka mkandarasi huyo kukabidhi mradi huo mwezi Mei kutokana na barabara hiyo kuwa msaada kwa mabasi yaendayo mikoa ya Kaskazini yakitokea kituo cha mabasi cha Magufuli.

Pia alikagua ujenzi wa daraja la Ulongoni A na B unaokwenda sambamba na ujenzi wa kingo za mto Msimbazi na kuonyesha kuridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo ambayo imefikia asilimia 70 hadi sasa na kuwataka wasimamizi kuikabidhi mwezi Juni.



Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, akikabidhi Sh. milioni 12 kwa wafanyakazi 11 wa kampuni ya Nyankiranganyi Constraction LTD, ambao walikuwa wamedhulumiwa na kampuni hiyo katika ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Geita jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Nani kurithi mikoba ya Bashiru CCM?

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kinatarajia kufanya Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa, Aprili 30, mwaka huu, ambao pamoja na mambo mengine utakuwa na jukumu la kumpitisha Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Mwenyekiti wa chama hicho.

Atakuwa mwanamke wa kwanza kwa CCM kuwa mwenyekiti tangu kuanzishwa kwa chama hicho.

Kwa mujibu wa Katiba ya CCM, anayechaguliwa kuwa rais ndiye anakuwa mwenyekiti wa chama hicho, na ikitokea amefariki anayeshika nafasi hiyo ndiye kiongozi.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli, alifariki Machi 17, mwaka huu, na kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, Makamu wake, alichukua madaraka ya kuongoza nchi.

Samia aliapishwa rasmi Aprili 19, mwaka huu, kuwa rais, na kinachofuata ni mchakato ndani ya chama kuwa mwenyekiti.

Macho na masikio ya Watanzania sasa ni kwa atakayeshika mikoba ya Dk. Bashiru Ally, aliyekuwa Katibu Mkuu, ambaye Hayati Magufuli wakati wa uhai wake alimteua kuwa Katibu Mkuu Kiongozi, akishika nafasi ya Dk. John Kijazi, aliyefariki dunia.

Rais Samia alimteua Dk. Bashiru kuwa mbunge na nafasi yake kushikwa na Balozi Hussein Athuman Katanga.

Baada ya mkutano mkuu kumpitisha kushika nafasi ya uenyekiti, atakuja na jina la Katibu Mkuu ambalo litapitishwa na wanachama.

Pia, kinachosubiriwa ni kujua majina ya wajumbe wa Sekretarieti, Katibu Itikadi na Uenezi, Naibu Katibu Mkuu na Makamu wenyeviti.

Kwa sasa kikatiba Makamu Mwenyekiti Zanzibar ni Rais Hussein Ali Mwinyi, na Makamu Mwenyekiti Bara, ni Philip Mangula, huku Katibu Itikadi na Uenezi, Hamprey Polepole ambaye pia ni mbunge wa kuteuliwa.

Kama ambavyo ilisubiriwa kwa hamu mabadiliko ya serikali ya Rais Samia, ndivyo inavyosubiriwa mabadiliko ndani ya chama, kwa kuwa anaruhusiwa kupanga safu yake ya uongozi itakayomsaidia.

Viongozi hao wataongoza kwa miaka mitano na katika uchaguzi Mkuu wa 2025, ambao utakuwa wa kwanza kwa rais aliyepo madarakani ambaye amepokea kijiti kwa mwezake kutokana na kufariki, na kikatiba Rais Samia ataruhusiwa kugombea nafasi hiyo.

Akizungumza wakati wa kuwaapisha mawaziri na manaibu Waziri, Rais Samia aliwaonya wanaoanza kuimendea 2025, na kwamba kwa sasa ni muda wa kufanya kazi.

Makatibu wakuu wa CCM waliopita na miaka waliyoongoza kwenye mabano ni Pius Msekwa (1977-1982), Rashid Kawawa (1982-1990), Horace Kolimba (1990-1995), Lawrence Gama (1995-1997), Philip Mangula (1997-2007), Yusuph Makamba (2007-2011), Wilson Mukama (2011-2012), Abdulrahman Kinana (2012-2018) na Dk. Bashiru 2018 hadi 2021.

# Viboko, mamba watishia maisha

**Na Gurian Adolf,** NKASI

DIWANI wa Kabwe wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Ahsante Lubisha, ameiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa haraka kibali ili Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ianze kuwavuna mamba na viboko katika kata yake litokana na kuwa tishio. Akizungumza na gazeti mwishoni mwa wiki, alisema viboko na mamba wamezaliana kwa wingi na kwa kuwa serikali imefanikiwa kudhibiti ujangili, na kwamba hivi sasa viboko wamekuwa wengi na wanazurura vijijini na wakikuta kuna nyumba ambayo mlango uko wazi wamekuwa wakiingia hadi ndani.

Alisema hali hiyo imezua hofu kwa wakazi wa vijiji vilivyopo katika kata hiyo, huku wakazi hao wakishindwa kutoka kwenda kwenye shughuli zao za kiuchumi kutokana na kuhofia maisha yao.

"Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita watu sita wameliwa na mamba akiwamo mwanafunzi Aidan Mwaloya(17) aliyeliwa na mamba hivi karibuni, alikuwa amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano na wengine kupata ulemavu wa kudumu," alisema.

Kaimu Ofisa Maliasili wa Wilaya ya Nkasi, Frank Wakungwa, alisema idara hiyo imeandika barua wizarani kuomba kibali ili wawavune kutokana na kuzurura maeneo ya vijijini kutoka Ziwa Tanganyika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Missana Kwangula, alisema kuwa hivi sasa kuna ongezeko kubwa la mamba na viboko katika kata kumi zilizopo mwambao wa Ziwa Tanganyika na wamekuwa hatari kwa maisha ya binadamu.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mwambe aipigia debe Benki ya CRDB uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amewataka Watanzania kuiunga mkono Benki ya CRDB kwa kupata huduma katika benki ili kuendelea kuiimarisha kwani inaonyesha uzalendo wa hali ya juu katika kuwainua wananchi kiuchumi.

Alisema hayo wakati wa semina ya uwekezaji na fedha iliyoandaliwa na Benki ya CRDB na kufanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watu zaidi ya 3,000, ambapo wengi wao walishiriki kupitia mtandao.

Alisema kwa benki hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia ajenda za maendeleo ya nchi na kuitaka kushiriki katika mkakati wa kupanua wigo wa uwekezaji nchini kwa kuanzisha dirisha maalum la viwanda ili kuchochea kuimarika viwanda vidogo na vikubwa kwa kuwawezesha wawekezaji kupata mitaji ya uhakika.

"Kwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hii Abdulmajid Nsekela ndio Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), nimuombe ashawishi na mabenki mengine kutekeleza hili. Nitaandaa mkutano na umoja huu ili uweze kulijadili hili kwa upana," aliongezea Mwambe.

Alisema Serikali kwa upande wake inaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa urasimu na kupunguza utitiri wa kodi na tozo ili kupunguza gharama za uwekezaji nchini ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mkurugenzi Mtendaji naomba nikuhakikishie mkiweza kuwawezesha wawekezaji hawa kuwekeza katika viwanda faida ni kubwa mno katika uchumi wa taifa letu. Tutaweza kuimarisha uchumi kwa kiasi kikubwa, ajira zitakuwa za kutosha, mzunguko wa fedha utaongezeka, na hata faida mtakayopata itakuwa zaidi ya hii Sh. bilioni 165", alisema Mwambe.

Waziri Mwambe aliainisha mpango wa Serikali ni kuachana na kusafirisha malighafi nje ya nchi kwa kutengeneza bidhaa hapa nchini kupitia viwanda vya ndani na kuzitafutia soko nje ya nchi. "Mfano kwa upande wa zao la pamba tumeweka mkakati ndani ya miaka mitatu hatutaki kuona tunauza pamba ghafi nje," alisema.

Aliipongeza hiyo kwa kuandaa Semina hiyo ya uwekezaji na fedha, huku akiwataka wananchi kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwekeza katika masoko ya mitaji ili kujijenga kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema malengo ya semina hiyo ni kuona Watanzania wengi zaidi wanashiriki katika fursa za uwekezaji hapa nchini pamoja na kupata uelewa wa huduma za benki hiyo zitakazowasidia kuwa wawekezaji wazuri.

Akielezea kuhusu program mbalimbali za elimu ya fedha na uwekezaji kwa umma, Nsekela alisema Benki ya CRDB ikiwa benki ya kizalendo inajivunia kwa kuwa mstari wa mbele katika kufikisha elimu ya fedha na uwekezaji kwa Watanzania.

Nsekela pia alimhakikishia Waziri Mwambe kuwa Benki hiyo itaendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi ili kujenga uwajibikaji wa kifedha katika jamii na kuongeza ujumuishi wa kifedha.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay, alimshukuru Waziri Mwambe kwa kuikaribisha benki hiyo kushirikiana na Serikali katika kutekeleza mikakati ya kuchochea uwekezaji nchini, ambapo alimhakikishia kuwa benki hiyo itakwenda kuandaa sera ambayo itakwenda kuelekeza na kusimamia uwezeshaji katika sekta ya viwanda na kuwa pendekezo la kuanzisha dirisha la viwanda limepokelewa kwa ajili ya utekelezaji.

# Total, Matata Foundation wafunguka kuhusu Samia

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya Mafuta ya Total Tanzania na Taasisi ya Flaviana Matata Foundation, zimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa rais na mwanamke wa kwanza kuliongoza taifa.

Wamesema, urais wa Samia umeipaisha nafasi ya Tanzania, kitaifa na kimataifa katika safari ya kuelekea kwenye usawa wa kijinsia kwenye uongozi wa kisiasa.

Mkurugenzi wa Mtandao wa vituo vya Mafuta vya Total nchinI, Marieme Sow, alitoa pongezi hizo wakati wa hafla fupi ya kukabidhi taulo za kike kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya Jangwani.

Katika kukabidhi taulo hizo kampuni hiyo, ilishirikiana na taasisi ya Flaviana Matata Foundation.

Sow alisema Total, imechangia ununuzi wa taulo hizo na kuzigawa bure kwa wanafunzi wahitaji kutoka familia maskini, kuwasaidia kuwa sawa na wanawake wengine.

"Kitendo cha Mama Samia kuwa rais wa kwanza mwanamke kwa Tanzania, na kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, urais wa Samia umeipaisha sana Tanzania katika anga la kimataifa, katika kuthibitisha Tanzania imepiga hatua kubwa kuelekea kwenye usawa wa kijinsia.

Sio kuthibitisha mwanamke ana uwezo sawa na mwanaume, bali kuthibitisha kuna wanawake wana uwezo kuzidi hata wanaume ila wamekuwa wanakosa fursa sawa kwa sababu tuu, wao ni wanawake, Rais Samia ni uthibitisho wa uwezo wa mwanamke."

Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Total Tanzania, Marsha Kilewo, alisema wanaamini uwezo wa wanawake na kuthamini mchango wa wanawake kwa maendeleo ya taifa, ndio maana imejiunga na Taasisi ya Flaviana Matata, kuunga mkono juhudi za kuwajengea uwezo sawa watoto wa kike.

Flaviana Matata, aliishukuru Total kwa kuunga mkono kampeni yake, kuwajali watoto wa kike.

Mwakilishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Hamza Hassan, aliipongeza Total Tanzania na Flaviana Matata Foundation, kusaidia watoto wa kike shuleni na kuzitaka taasisi nyingine kuiga mfano huo kwa sababu bado shule zinakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Jangwani, Mwalimu, Paulina Aweda, aliishukuru msaada huo na kusisitiza usiwe kwa watoto wa familia masikini, bali kwa hata waliopo shuleni ambao hupatwa na hali ya siku zao ghafla shuleni.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)**
**Dar es Salaam, Aprili 08, 2021**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Simba waandaliwa namna ya kunufaika na VAR

**MABINGWA** wa Ligi Kuu Bara, Simba kwa sasa wanachosubiri ni kujua mpinzani wao wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye droo itakayochezeshwa Aprili 30, mwaka huu jijini Cairo, Misri yalipo makao makuu ya Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Simba imetinga hatua hiyo ikiwa kinara baada ya kuongoza Kundi A, ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri ambao nao wamefuzu baada ya kushika nafasi ya pili wakiwapiku AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan iliyoburuza mkia.

Na kwa mujibu wa kanuni za waandaaji wa michuano hiyo, CAF, vinara wa makundi kutoka kila kundi watakutana na timu zilizoshika nafasi ya pili, lakini zilizokuwa katika kundi moja hazitakutana kwenye hatua hii, huku pia washindi wa pili wakianzia nyumbani.

Hivyo, Simba sasa kuna uwezekano wakukutana na CR Belouizdad au MC Alger za Algeria ama Kaizer Chief ya Afrika Kusini, huku Al Ahly ikiwa na nafasi ya kukutana na Wydad Casablanca ya Morocco, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini au ES Tunis ya Tunisia.

Hata hivyo, tofauti na hatua ya makundi, kuna taarifa kuwa kuanzia robo fainali CAF inataka Teknolojia ya Video ya Kumsaidia Refa (VAR), ianze kutumika tofauti na msimu uliopita ambapo ilitumika kwenye mechi ya fainali pekee.

Nipashe tunatambua kuna faida kubwa ya VAR katika kuhakikisha haki inatendeka kwa refa kutoa maamuzi sahihi ambayo hayataegemea upande wowote ule na hivyo mwisho wa siku kupatikana bingwa halali.

Lakini pia tunatambua itakuwa ni mara ya kwanza kwa Klabu ya Simba kucheza na VAR, ingawa kwa wachezaji, tunaamini kuna baadhi ambao huenda walishacheza katika hali kama hiyo katika maisha yao ya soka wakiwa na klabu nyingine ama timu zao za taifa. Kutokana na hilo, ni wazi kuna haja ya Klabu ya Simba kutoa darasa kwa wachezaji wao namna ya kuweza kunufaika na VAR, kwani wachezaji wakiwa uwanjani ndio wanaoweza kumshawishi refa kwenda kupata uhakika wa tukio husika kwenye VAR ama kulipotezea.

Kama wachezaji wasipojenga utamaduni wakulalamika kwa kunyosha mikono ili kumshawishi refa kwamba kuna madhambi yamefanyika ambayo hakuyashuhudia, ni wazi kama pia mwamuzi hakujulishwa kwa alamu na wasaidizi wake wa pembeni, atapotezea tukio husika.

Tunatambua Simba ina wachezaji wengi ambao wanauwezo mkubwa wa kukokota mpira na kuingia nao kwa kasi ndani ya boksi, jambo ambalo ni rahisi sana kwa timu pinzani kuwachezea madhambi na kusababisha faulu, hivyo kama wachezaji hawatajenga utamaduni wa kulalamika bila kumbughudhi mwamuzi, ni wazi watakuwa wanakosa nafasi nyingi za kunufaika na VAR.

Tunafahamu wachezaji wa Simba wanafuatilia sana soka la kimataifa na wanajua vema namna gani ambavyo wanzao hutumia VAR kunufaika na teknolojia hiyo kwa kumlalamikia mwamuzi bila kujisababishia kadi, lakini pia pamoja na ufahamu wao huo, kuna haja ya kuandaliwa darasa na kuongeza pia umakini kwa upande wao.

VAR inapotumika wachezaji wengi hulazimisha kusababisha makosa kwa wapinzani ili kuweza kunufaika na teknolojia hiyo kwa kwenda kumshawishi mwamuzi wa kati kwamba kuna madhambi yamefanyika, hivyo Simba wanapaswa kulifahamu hilo na kutambua kwamba teknolojia hiyo pia itang'ata pande zote.

Tunachotaka kukishuhudia msimu huu, ni kuona Simba ikifika fainali na hata kutwaa ubingwa huo, jambo ambalo si tu watajiwekea rekodi kama klabu, bali kubwa zaidi ni soka la Tanzania kutangazika zaidi kimataifa, hivyo kuna haja sasa ya kuanza kujipanga mapema kwa kila kitu ndani na nje ya uwanja kabla ya hatua ya robo fainali mwezi ujao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanayanga sasa wamejua uongo hupanda kwa lifti, ukweli kwa ngazi

Na Adam Fungamwango

**INAWEZEKANA** kuna baadhi ya watu ndani ya Yanga walifanya hivyo kwa makusudi ili kuuchelewesha ukweli. Lakini hii haikuwa kwa manufaa ya klabu, bali yao binafsi.

Mwanamuziki Koffi Olomide kwenye moja kati ya mamia ya nyimbo zake, anasema uongo hupanda lifti, lakini ukweli hupanda ngazi. Hii ina maana uongo utawahi kufika kabla ukweli. Na ndivyo ilivyo kwenye maisha ya walimwengu.

Watu huuamini sana uongo. Na ndiyo unaoaminika zaidi kuwa ukweli. Hata hivyo, siku zote ukweli ambao hupanda ngazi, hata kama ni baada ya miaka 100, utafika tu.

Hapa duniani ukweli utajulikana tu na uongo lazima ujulikane, hata kama vyote vilifichwa kwa miaka gani. Ndiyo maana waswahili wana msemo wao wa 'panapo ukweli, uongo hujutenga.

Kuna watu Yanga walificha ukweli ambao kwa sasa umeanza kudhihirika. Imetumika nguvu nyingi na gharama kuuficha ukweli huo. Wamejitahidi sana.

Lakini kama ilivyo kanuni za ukweli na uongo.

Ni kwamba ukweli ni lazima utajulikana tu, haijalishi ni miaka mingapi.

Baada ya usajili kuna watu walio ndani ya Yanga waliwaaminisha wanachama na mashabiki kuwa wamesajili wachezaji bora, mahiri na wenye viwango vya juu kuliko timu yoyote ile nchini.

Ligi ilianza kama kawaida. Yanga ilianza kushinda. Lakini si kwa vile ambavyo waliambiwa kutokana na viwango vya wachezaji walioambiwa. Wale watu wanatengeneza propaganda kuwa timu bado haina muunganiko. Timu iliendelea kushinda, lakini bila kiwango kilichotarajiwa, yakatengenezwa mazingira kuwa kocha Zlatco Krmpotic hana uwezo, akatimuliwa.

Kiwango cha uchezaji kikawa ni kile kile. Wakati mwingine timu inashinda, wakati mwingine inasuasua. 'Wachawi' sasa wakawa waamuzi na tamko likatoka kuwashutumu kuwa wanainyonga Yanga. Baadaye tena ikahama kutoka kwa waamuzi, sasa lawama zikapelekwa kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi yake.

Lakini wakati lawama zikipelekwa huko, Yanga ikamtimua kocha mwingine Cedric Kaze, hali iliendelea kuwa ile ile. Panapo ukweli uongo hujitenga.

Minong'ono sasa ikaanza kutoka kwa Yanga wenyewe kuwa baadhi ya wachezaji waliosajiliwa, hawakupaswa kuichezea timu hiyo.

Huu ndiyo ukweli mchungu ambao Yanga ilipaswa kuuzungumza awali kwa ajili ya kujenga timu, lakini walikuwa wanakwepa. Zile lawama zilipokuwa zinakwenda huku na huko ilikuwa ni kupoteza lengo. Sasa kila mmoja anaongea hilo.

Kiungo wa zamani wa Yanga, Sekilojo Chambua, amewataka viongozi wa Yanga kuangalia upya mfumo mzima wa usajili kwenye klabu hiyo ili kuleta wachezaji wenye uwezo mkubwa na tija kwenye timu.

Chambua aliyetamba na Yanga kuanzia katikati ya miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 amesema imefika wakati sasa viongozi kuwatumia watu sahihi ikiwamo wachezaji wa zamani kufanya usajili kuliko ilivyo hivi sasa.

Kiungo huyo amekuwa ni mmoja kati ya wanachama, wachezaji wa zamani na mashabiki wa Yanga kulalamikia uwezo wa wachezaji timu hiyo baadhi yao ni mdogo kwa timu kubwa kama hiyo kiasi cha kuifanya isifanye vizuri.

Aliungana na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, ambaye anafunguka na kusema Yanga ina baadhi ya wachezaji ambao hawajitumi na wengine hawana uwezo wa kuichezea timu hiyo.

Muro ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga, alishangazwa kuona timu kubwa kama Yanga kuwa na mastraika ambao wana miezi mitano na wengine mwaka bila kufunga bao, na akaongeza kuwa hiyo siyo kama anayoijua yeye ya 'kampa kampa tena.'

Beki wa zamani wa klabu hiyo, Bakari Malima 'Jembe Ulaya' naye pia aliibuka na kudai anachokiona ni kwamba kila siku zinavyozidi kusonga mbele ndiyo viwango vya wachezaji wa Yanga vinaonekana kuzidi kuporomoka.

Huu ni ukweli mchungu ambao Wanayanga walipaswa kuusema mapema, licha ya kwamba kuna baadhi ya wachezaji hao walipokewa kwa mbwembwe kubwa Uwanja wa Ndege.

Kwa sasa wamechelewa, hivyo wasubiri ligi imalizike, wawaondoe baadhi ya wachezaji mizigo kwenye klabu yao hata kama walishangiliwa na kubebwa kuanzia Uwanja wa Ndege hadi klabuni.

# HABARI KITAIFA

## Wakulima kukopeshwa zana bila dhamana

**Na Beatrice Shayo**

KAMPUNI ya Pass Leasing Company Ltd imesema itaanza kutoa mikopo ya zana za kilimo na viwanda bila dhamana kwa masharti nafuu, kuwawezesha wakulima kuongeza tija na thamani ya mazao wanayozalisha.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Killo Lusewa, na kwamba wameshapatiwa kibali cha uanzishaji shughuli za mikopo ya zana na vifaa mbalimbali vya kilimo.

Lusewa alisema dhamira ya kampuni hiyo ni kuhakikisha wazalishaji wa sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji wanakuwa na uwezo wa kupata zana bora na za kisasa kwa kupitia mpango wa kukodishwa ama kukopeshwa vifaa kwa bei nafuu.

"Watu tunaowalenga ni wakulima na wajasiriamali wanaojishughulisha na kilimo kwa ujumla kikiwamo kilimo cha mazao, umwagiliaji, uvuvi, ufugaji wa wanyama na nyuki, misitu, usafirishaji, uhitaji pamoja na usindikaji wa vyakula," alisema.

Alisema kupitia kampuni yao wateja watanufaika na huduma bora kwa kuhudumiwa na wataalamu waliobobea kwenye sekta ya mikopo na kilimo, wateja watapata huduma kwa wakati, mteja atamiliki vifaa kwa gharama nafuu na bila kuweka dhamana yoyote.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PASS TRUST, Anna Shanalingigwa, alisema Taasisi ya Private Agricultural Sector Support (PASS), ilianzishwa mwaka 2000 chini ya programu ya kusaidia sekta binafsi ya kilimo kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha na biashara kwa wajasiliamali wa bidhaa na huduma katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nchini Tanzania.

## Mashirika ya kuhudumia kambi za wakimbizi yakumbushwa wajibu

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MASHIRIKA ya kuhudumia wakimbizi Mkoa wa Kigoma, yametakiwa kutekeleza sheria ya utengaji fungu la fedha za kusaidia miradi ya maendeleo katika vijiji jirani vinavyozunguka kambi za wakimbizi.

Akizungumza wakati wa kupokea jengo la choo na mradi wa majisafi na salama katika Shule ya Msingi Nyamuganza, kijiji cha Nyamidaho, wilayani Kasulu, miradi iliyotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Save the Children, Ofisa elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Respice Swetu, kwa niaba ya Mkurugenzi wa wilaya hiyo, Joseph Kashushura, aliyataka mashirika yanayoshindwa kutekeleza sheria hiyo kuacha mara moja.

Alisema baadhi ya mashirika hayajafanya vizuri kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi wanaozunguka kambi za wakimbizi jambo ambalo si sawa kwa kuwa wanatakiwa kutenga fungu maalum kwaajili hiyo, lakini bado kumekuwapo na baadhi ya mashirika yasiyotekeleza.

Mratibu wa mradi wa elimu kuoka Shirika la Save the children, Jackson Nsabo, alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa mtoto, shirika lilikusudia kuendelea kusaidiana na serikali na kuunga mkono juhudi za kutoa elimu na ulinzi kwa mtoto katika maeneo yanayozunguka kambi za wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma.

Alisema walianza kujenga vyumba vya madarasa vitatu katika shule mbili za msingi zilizopo katika Wilaya ya Kibondo, na kwamba wapo hapo kukabidhi miundombinu ya majisafi na salama kwa kujenga tangi lenye ujazo wa lita 10,000 na sehemu maalum ya kunawia mikono katika Shule ya Msingi Nyamuganza, ikiwa ni uwakilishi wa shughuli zilizofanyika katika wilaya ya Kibondo na Kasulu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Goodluck Kibanda,- alisema shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 965 inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo upungufu wa vyumba 17 vya madarasa na vilivyopo ni vyumba vinne vinavyotumiwa na wanafunzi wa awali hadi darasa la saba.

Pia upungufu wa matundu 13 ya choo, madawati 122 na walimu 13, waliopo ni wanane pamoja na tatizo la ukosefu wa nishati ya umeme.

## Wadau waombwa kuchangia ujenzi wodi wajawazito

**Na Neema Sawaka**

WADAU mbalimbali katika kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wameombwa kujitokeza kusaidia ujenzi wa wodi za kujifungulia.

Kwa sasa wajawazito wanalazimika kutembea umbali wa kilomita nane kufuata kituo cha afya cha Mbika ili kupata huduma hiyo kwa kuwa zahanati katika eneo hilo ina chumba kimoja na kitanda kimoja.

Muuguzi wa zahanati ya kijiji cha Kangema kutoka kata hiyo, Theresia Aloyce alitoa ombi hilo jana wakati wa makabidhiano ya msaada wa tani moja ya saruji iliyotolewa na benki ya CRDB tawi la Kahama mjini.

Theresia alisema wajawazito wamekuwa wakikataa kupata rufaa kwenda katika hospitali zingine kutokana na umbali mrefu na hivyo baadhi yao kujifungulia nje ya wodi ya wazazi na wengine njiani.

"Kwa siku wajawazito wanne hadi watano hujifungua na mwezi hufikia wajawazito 40, lakini wodi ya wazazi ikikamilika huenda ikafika mpaka wajawazito 70 tunalazimika kuwapatia rufaa, lakini baadhi yao hung'ang'ania na kujifungulia chini jambo ambalo ni hatari kwa kuwa linaweza kupoteza maisha mama na mtoto," alisema Theresia.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Dk. Mshahara Mpuya, alisema ukosefu wa wodi ya wazazi umewalazimu kuwapatia rufaa wajawazito kwa kwa sababu chumba cha kujifungulia kipo kimoja na kifinyu.

Diwani wa kata hiyo, Gabriela Kimaro alisema zahanati hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa chumba cha kujifungulia na kuwafanya wajawazito kupewa rufaa wakiwa hawana tatizo lolote na wengine hukataa na hivyo kulazimika kujifungulia chini.

"Zahanati hii inahudumia wagonjwa wengi wengine kutoka nje ya kata ya Ulowa yenye wakazi zaidi ya 200,000 na vitongoji 36.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Michael Matomora, alisema saruji hiyo ataikabidhi kwa mwenyekiti wa kijiji ambaye atasimamia ujenzi ili kuondokana na ukosefu wa wodi ya wazazi. Meneja wa benki ya CRDB tawi la Kahama, Evodi Kereti, alisema wameamua kutoa msaada wa Sh. milioni nane na tani moja ya saruji kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa wodi ya wazazi katika zahanati hiyo.


NMB Karibu yako

**MABORESHO YA MAWASILIANO NA TAARIFA ZA KIBENKI KWA WANAHISA WA BENKI YA NMB KWA AJILI YA MALIPO YA GAWIO**

Benki ya NMB Plc inaendelea na juhudi za kuhakikisha wanahisa wetu wanaridhika na huduma zetu na malipo ya gawio kwa wakati. Gawio hulipwa kupitia akaunti za benki za wanahisa. Tunaomba wanahisa wote wa NMB waboreshe taarifa za mawasiliano yao na taarifa za kibenki kwa ajili ya akaunti zao husika watakazotumia kupokea gawio.

Hii ni kwa wanahisa pekee wa NMB;

i. Ambao hawajawahi kupata gawio lolote tangu waliponunua hisa
ii. Ambao waliobadilisha akaunti zao za kupokelea gawio na hawajaiarifu benki (Ikiwa ni pamoja na wanahisa wapya).
iii. Ambao wamebadilisha anwani zao za mawasiliano (namba za simu au anuani ya makazi)
iv. Ambao akaunti zao zimelala (Dormant) au kufungwa

Tafadhali tembelea tawi la NMB lililo karibu nawe na ujaze kwa usahihi fomu ya gawio la mwanahisa, na kisha uiwasilishe pamoja na kitambulisho na cheti cha hisa kwa dawati la huduma kwa wateja au tuma kama barua au barua pepe katika anuani zifuatazo hapo chini:

NMB Plc – Makao Makuu | Ohio/Ali Hassan Mwinyi
Ghorofa ya nne - Idara ya Fedha na Taarifa
S.L.P 9213, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 222 322 000 | Nukushi: + 255 222 112 148

**Kwa maelezo Zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia:**
Barua Pepe: Dividend_Unit@nmbbank.co.tz Au
wasiliana moja kwa moja na:

- Njabha Njabha - Simu namba 0222 322 356
- Lucky Kyando - Simu namba 0222 322 421
- Robert Mwita - Simu namba 0222 322 376

www.nmbbank.co.tz

## Wanafunzi, wajasiriamali wanawake wakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Kibiti mkoani Pwani imenufaika kwa msaada wa madawati wa elimu na ujasiriamali. Imekabidhiwa madawati 250, viti pamoja na meza 250, huku wajasiriamali wanawake wakijengewa uwezo.

Msaada huo umetolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ikiwa ni sehemu ya Mpango wa uwajibikaji wa Jamii ambao unalenga kuchangia utoaji wa elimu bora nchini.

Kadhalika, benki hiyo pia imetoa mafunzo ya kibiashara na ujasiriamali kwa wanawake wajasiriamali 150 wilayani humo ili kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara zao kwa ufanisi, huku wakizingatia nidhamu ya fedha kabla hawajapatiwa mikopo kwa ajili ya kukuza mitaji yao. Madawati hayo yalikabidhiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo wa benki hiyo, Elibariki Masuke, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Gullamhussein Kifu. Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Mbunge wa Kibiti, Twaha Mpembenwe na maofisa wengine wa wilaya hiyo akiwamo mkurugenzi mtendaji.

Masuke alisema benki hiyo imejitolea kusaidia katika kuboresha ustawi wa jamii kupitia misaada ya kijamii ikiwamo elimu, na kwamba wameguswa sana na suala la changamoto ya madawati kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini hivyo kuchukua hatua hiyo kuboresha zaidi sekta hiyo.

"Ni furaha kwetu kuwa sehemu ya kutatua changamoto kwenye sekta muhimu kama hii. Kupitia ushirikiano na ushawishi tunaoupata kutoka kwa Mbunge wa Kibiti na ofisi ya Mkuu wa wilaya tunaahidi kuendelea kushirikiana na jamii ya wana Kibiti huku pia tukifikiria namna kufungua tawi letu wilayani Kibiti kufuatia fursa mbalimbali tunazoziona ikiwamo kilimo na mradi wa kituo cha kupozea umeme wa Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere,'' alisema. Kuhusu mafunzo kwa wajasiriamali wanawake, Masuke alisema miongoni mwa sababu zinazokwamisha utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wengi ni pamoja na wao kuendesha biashara zao bila kuzingatia misingi ya kifedha ikiwamo kutunza kumbukumbu za mahesabu ikiwemo mapato na matumizi.

Kwa mujibu wa Masuke changamoto hiyo ndio sababu benki imekuwa ikishirikiana na taasisi nyingine kama TanTrade, SIDO, VETA na washauri binafsi kuelimisha wajasiriamali kuhusu namna bora ya kusimamia na kuendesha biashara zao ili kuwajengea uwezo kabla ya kuwapatia mikopo.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kifu pamoja na kuishukuru benki ya NBC, aliiomba ifungue tawi lake wilayani humo mapema iwezeknavyo ili kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara hususani wadogo.

Akizungumzia mafunzo kwa wajasiriamali wanawake Kifu alitoa wito kwa washiriki kuhakikisha wanayatumia vyema na kuwa yanalenga kuwasaidia katika upatikanaji wa mikopo sambamba na kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kwa faida.

Kwa upande wake Mbunge Mpembenwe aliiomba benki hiyo iendelee kuwekeza zaidi wilayani humo kwa kufungua tawi lake sambamba na kuwasaidia wajasiriamali na wakulima hususani wa zao la ufuta pamoja na vijana ambao wanakibiliwa na changamoto ya huduma za kifedha.

# Kaya 320 zazingirwa na maji

**Na Gurian Adolf,** NKASI

KAYA 320 katika Kata ya Kirando mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani Nkasi mkoani Rukwa zimebaki bila makazi kutokana na kuzingirwa na maji.

Hayo yalibainishwa na Diwani wa Kata ya Kirando, Kakuli Seba, alipozungumza na Nipashe, wakati wa kikao cha baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ,kilichofanyika mwishoni mwa wiki katika Mji Mdogo wa Namanyere.

" Nyumba 320 ambazo ni za kisasa zimezingirwa na kujaa maji katika vijiji vya Mtakuja na Kichangani na kusababisha wananchi kuzikimbia nyumba zao," alisema.

" Kila upepo wa Kaskazi unapovuka ujazo wa maji ziwani unaongezeka na kusababisha mafuriko ambayo yanapeleka maji vijijini na nyumba za wakazi wa vijiji hivyo zinajaa maji pia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Missana Kwangula, alisema viwanja vya makazi vimetengwa na kupimwa jirani na eneo la Shule ya Sekondari Nkasi ili vigawiwe kwa waathirika wa mafuriko ya maji ya Ziwa Tanganyika.

Alisema eneo hilo liko katika ukanda wa juu, lakini changamoto iliyopo ni mwamko mdogo wa wananchi kuhamia na kujenga makazi yao kutokana na kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii.

Aliongeza kuwa pia ofisi ya Serikali na mwalo wa samaki umezingirwa na kujaa maji, hivyo kuna changamoto kubwa kwa wananchi hao kupata baadhi ya huduma.




Kaimu Afisa Tawala Wilaya ya Mufindi - Joseph Mchina akimkabidhi Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Isupilo Patrick Mwageni msaada wa Meza kwa ajili ya Walimu zilizotolewa na Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu. Wengine ni Meneja wa NMB Mufundi – Mary Mpasha (Kushoto mwenye miwani) na Katikati ni Meneja wa NMB Nyanda za Juu – Straton Chilongola (Miwani).NMB ilitoa madawati, Mabati kwaajili ya shule nne za msingi vyenye thamani ya shilingi Milioni 17.3

# Watendaji waagizwa kukusanya taarifa ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, imewaagiza watendaji wa vijiji kukusanya taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwenye maeneo yao na kuziwasilisha katika ngazi za uamuzi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Msalala, Neema Katengesya, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na maofisa watendaji wa vijiji, kamati za Mtakuwwa na vikundi vya kinamama vya kupinga ukatili wa kijinsia (WGF), katika warsha ya siku moja iliyofanyika kata ya Bugarama.

Alisema kuwa maofisa hao wanatakiwa kutimiza wajibu wao kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kukusanya taarifa za vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto chini ya miaka 18.

"Kesi nyingi za vitendo vya ukatili wa kijinsia katika halmashauri hii zimedaiwa wahusika wanakutana na kumalizana kwenye ofisi za vijiji na wala hazipelekwi kwa maofisa maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii, dawati la jinsia wala mahakamani," alisema Katengesya.

Naye Ofisa ustawi wa jamii wa halmashauri hiyo, Asnath Remtula, alisema Mkoa wa Shinyanga unaoongoza kwa vitendo vya ukatili.

Ofisa ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa Shirika la Rudi Kahama, Leticia Shilinde, aliwataka watendaji wa vijiji kujitoa kusaidia jamii wanayoitumikia hasa upatikanaji wa taarifa sahihi zinazoendelea kwenye vikundi ili kutokomeza vitendo hivyo.

Mkurugenzi wa Shirika la Life Securing and Relif Services (LSRS), Bwire Denisy, alisema wanatekeleza mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto (DRR II) katika Halmashauri ya Msalala kwa kushirikiana na Shirika la Rudi Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la OXFAM Ubelgiji.

HABARI KITAIFA

# Kesi 61 za 'unga' zaripotiwa mkoa mmoja kwa miezi 24

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya kesi 61 za dawa za kulevya zimeripotiwa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuanzia Januari 2019 hadi Disemba 2020.

Kesi hizo zinahusu bangi na dawa aina ya heroin, ambazo ziliripotiwa mwaka 2019 ni 28 na mwaka 2020 kesi 33.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alisema wataendelea kupambana ili kuhakikisha madawa ya kulevya hayaingizwi katika mkoa huo.

Alisema Jeshi hilo linaendelea kuwaonya wananchi wanaojihusisha na uuzaji, uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya na kwamba halitomvumilia mtu yeyote atakae bainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Alieleza ni kosa kisheria kuingiza, kuuza na kutumia dawa za kulevya, hivyo atakaebainika kujihusisha na dawa za kulevya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Kamanda huyo alisema mwaka 2020 kesi zimeongezeka kuliko mwaka 2019, hivyo wataendelea kufanya msako ili kuhakikisha mwaka huu zinapungua.

"Mikakati yetu ni kwamba tumejipanga vyema katika kukabiliana na makosa haya, ili kuhakikisha tunapunguza kasi ya makosa hayo ama tunaondoa kabisa," alisema.

"Tunaendea kufanya misako ya mara kwa mara katika maeneo yote ya mijini na vijijini, ili kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na uuzaji, uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya bila ya kuwaonea aibu," alisema Kamanda Sadi.

Mikakati mingine waliojiwekea Jeshi hilo ni kuendeleza vikao na kuwapa taaluma wapelelezi wa makosa hayo, ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi yao kwa ufanisi na uweledi zaidi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari ya dawa za kulevya.

Aliwataka wanachi kujiepusha na vitendo hivyo kwani athari zake ni kubwa na hupelekea kupoteza nguvu kazi ya Taifa, kudumaza uchumi, kusababisha ongezeko la maradhi, uhalifu na kuharibu maadili kwa jamii kwa kuiga vitendo visivyofaa.

Kukamatwa na dawa za kulevya ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 13 (d) cha Sheria ya Udhibiti wa dawa za kulevya, sheria namba 9 ya mwaka 2009, sheria ya Zanzibar kama ilivyorekebishwa na sheria namba 12 ya mwaka 2011.

## Tigo, TAPSOA kuwezesha wateja malipo ya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania imeungana na Umoja wa Waendeshaji wa vituo vya mafuta nchini (TAPSOA) ili kuwawezesha wateja kulipia mafuta kwa kutumia Tigo Pesa.

Malipo hayo ni kupitia namba 777512, na kwamba uzinduzi wa huduma hiyo ni mwendelezo wa maadhimisho ya miaka 10 ya Tigo Pesa nchini.

Afisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo, Angelica Pesa, alisema: "Tanzania inahitaji huduma za kibunifu zinazolega kutatua changamoto za kila siku. Katika kusherekea miaka 10 ya Tigo Pesa, tumekuja na suluhu la muda mrefu kwa wamiliki wa vyombo vya moto nchini."

Pesha aliongeza: "Kama kampuni ya kidigitali tunaamini muungano huu kati ya Tigo na TAPSOA utaondoa msongamano kwenye vituo vya mafuta nchini. Tunawasihi wateja kutumia huduma hii ili kurahisisha malipo ya mafuta katika vituo mbalimbali."

Ili kufanya malipo, mteja wa Tigo Pesa atapiga *150*01# na atachagua 4, kulipa bili, ingiza namba ya malipo 777512 kisha namba ya kituo cha mafuta, ingiza kiasi na kisha namba ya siri ya Tigo Pesa.

"Ni matumaini yetu kuwa kupitia Tigo Pesa tumerahisisha malipo ya mafuta kwa wamiliki wa vyombo vya moto kwani kwa sasa hakuna tena haja ya kutembea na pesa taslimu, kwa simu yako tu unakuwa na uhakika wa kupata mafuta katika kituo chochote nchini," alisema Pesha.

Katibu Msaidizi kutoka TAPSOA, Maulid Mahfudh, alisema wao wana furaha kuungana na Tigo, kwani huduma ya Tigo Pesa ni ya uhakika na ni rafiki kwani inaweza kutumika mahali popote na wakati wowote na kuwataka wamiliki wa vituo vya mafuta kujisajili ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wateja.

"Tunafuraha kubwa kuungana na Tigo Pesa na napenda kuwahakikishia kuwa vituo vyote vya mafuta nchini vitahakikisha wateja wanafanya malipo kwa njia ya Tigo Pesa. Katika kuadhimisha miaka 10 ya Tigo Pesa nawapongeza Tigo kwa kuanzisha huduma hii ambayo imekuwa na umuhimu mkubwa hapa nchini," alisema.




Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya TPB, Henry Bwogi (wanne kulia), akikabidhi mahitaji maalum kwa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Ekwabi Majugu (watatu kushoto). Msaada huo ni kwa ajili ya kambi ya wanafunzi wa kidto cha 4 na 6 katika Mkoa wa Simiyu. Hafla hiyo ilifanyika katika Shule ya Sekondari Bariadi mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako mifuko ya plastiki waendelea

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema kuwa linaendelea kuwasaka wazalishaji na watumiaji wa vifungashio ambavyo havijathibitishwa kisheria, na kwamba Aprili 19, itatoa tathmini ya msako huo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliyasema hayo jana akizungumza na Nipashe kuhusu msako huo ambao ulianza tangu Aprili 9, mwaka huu.

"Jumatatu (Aprili 19), tutaonyesha kila kitu ambacho tutakipata kwenye msako, ingawa hatujamkata yeyote hadi sasa," alisema Dk. Gwamaka.

Pia mkurugenzi huyo akiwa katika mkutano wa wadau mbalimbali ikiwamo wenye viwanda, mwishoni mwa wiki, alisema uzalishaji wa vifungashio viliruhusiwa kisheria nchi unaridhisha, hivyo kusiwe na sababu ya kuendeleza matumizi ya vifungashio vilivyokatazwa.

Dk. alibainisha kwamba, kwa ambao watakiuka katazo la matumizi ya mifuko hiyo, adhabu yake ni pamoja na faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi 200,000 kutegemeana na kosa.

Kadhalika, alisema wazalishaji wakubwa wa bidhaa za vifungashio vya plastiki ikiwamo viwanda adhabu ni faini ya Sh. milioni tano hadi Sh. bilioni 10 kutegemeana na aina au ukubwa wa kosa.

"Desemba 31, mwaka jana, NEMC, tulikumbusha kuhusu kanuni kwamba ilisema vifungashio ambavyo havijakidhi vigezo visionekane katika mazingira. Ili kwa wanaotumia vifungashio na kutengeneza kwa wingi wasajiliwe au kupewa maelekezo," alisema Dk. Gwamaka. Alisema lengo la kanuni na katazo hilo ni kulinda mazingira na kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Dk. Gwamaka alisema kanuni iliwekwa ili kulinda mazingira, kupunguza uchafuzi kutokana na mifuko ya plastiki ambayo haiwezi kurejelezwa ambayo haiozi isiyooza ardhini kwa takribani miaka 400 hadi 500."

"Tarehe 8, Januari mwaka huu, waziri wa nchi ofisi ya makamu wa rais, alionyesha huruma na kuongeza muda wa matumizi ya mifuko hii, sheria inakataza ndio maana wakapewa miezi mitatu, kusiwe na bidhaa ambayo TBS (Shirika la Viwango Tanzania) haijaruhusu, haijasiliwa na kuwa sokoni.

Kadhalika, Dk. Gwamaka aliwataka wenye viwanda na wajasirimali wa bidhaa za vyakula, mifugo na kilimo kuanza kujiandaa kutumia vifungashio mbadala rafiki wa mazingira, ili kuepuka adhabu.



Meneja kutoka kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Kanda ya Ziwa, Pendo Gondwe (mwenye koti jeusi), akiwa na maofisa kutoka kituo hicho, kwenye ziara ya kiwanda cha Jambo mkoani Shinyanga na kuangalia shughuli za uzalishaji bidhaa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanachama sita ACT wachiwa huru

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANACHAMA sita wa Chama cha ACT-Wazalendo Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, waliodaiwa kuharibu mali za Ofisi ya Kata Mji Mdogo wa Kivinje, wameachiwa huru.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya kukosekama ushahidi ambao ungeiwezesha mahakama kuwatia hatiani kwa makosa yaliyokuwa yakiwakabiri.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Conslata Singano, kufuatia upande wa mashtaka kushindwa kuwasilisha ushahidi wake.

Wanachama walioachiwa huru na Mahakama hiyo ni Mwanahamisi Bakari Arobaini (39), Zidadu Said Nango (55), Said Korosheni Huseni (44), Muhusini Ally Mohamedi (44), Jabiri Salum Mbio (44) na Sharifa Said Bungara (35) wote ni wakazi wa Kata ya Mji Mkongwe wa Kivinje, wilaya ya Kilwa.

Wanachama hao walifikishwa katika Mahakama ya Mkoa, wakikabiliwa na kesi ya kuharibu mali ya Ofisi hiyo ya Kata ,ni viti (35), mabenchi (3) na meza mbili vyote vikiwa na thamani ya Sh,940,000/-mali za Ofisi ya Kata ya Kivinje.

Kabla ya kutolewa kwa uamuzi wa kuwaachia huru washitakiwa hao, wakili Rainery Songea aliyekuwa akiwatetea wanachama hao akaiomba Mahakama kuliondoa Shauri hilo, kwa madai upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa ambalo wateja wake wameshitakiwa nayo.

"Mheshimiwa Hakimu, kutokana na upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa, naiomba Mahakama yako tukufu kuliondoa shauri hili," aliomba Songea.

Hakimu Singano akiifuta shauri hilo namba 29/2020, alisema analikubali maombi la wakili Songea, akiifuta kupitia kifungu 230 sura ya 20 marekebisho 219 (CPA), aliwaachia huru washitakiwa wote sita bila masharti mengine.

"Kwa vile upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa mbele ya Mahakama hii, washtakiwa wote mnaachiwa huru nendeni majumbani mwenu, "alimazia Hakimu Singano.

Awali ilidaiwa Mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Abdurahamani Mohamedi, kuwa washtakiwa hao walidaiwa kuharibu mali hizo za Ofisi ya Kata zenye thamani ya Sh. 940,000 Oktoba 29/2020 siku moja baada ya kufanyika uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na Rais.

# Kiwanda chataka udhibiti wa bidhaa za nje

**Na Joseph Mwendapole**

KIWANDA cha kutengeneza kanga, vitenge na nguo za aina mbalimbali cha NIDA kimeiomba serikali kudhibiti bidhaa zinazotoka nje ya nchi zilipe kodi zote stahili ili kulinda viwanda vyake vya ndani.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa kiwanda hicho kilichoko barabara ya Mandela, Muhamad Hassaan, wakati wa ziara ya maofisa wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Maofisa hao walifanya ziara kiwandani hapo kuangalia utendaji wake na changamoto wanazokabiliana nazo ili zipatiwe ufumbuzi.

Hassaan alisema kuna bidhaa zinazozalishwa kwa gharama nafuu zinazotoka nje ya nchi hivyo kama zitaachwa ziingie kwenye masoko ya Tanzania yanahatarisha uhai wa viwanda vya ndani.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa kikiongeza uzalishaji mwaka hadi mwaka na kwasasa kinashirikiana na wakulima kulima zao la pamba Wilaya ya Kahama Shinyanga.

Alisema wamekuwa wakiwasaidia wakulima hao kulima kisasa na kuwapa pembejeo na baadaye wamekuwa wakinunua zao hilo wao wenyewe hivyo wakulima hao kuwa na uhakika wa soko.

Alisema wanatarajia kuanza kuingia kwenye masoko ya Ulaya na Marekani na kwa sasa wanauza bidhaa zao kwenye nchi za Afrika Mashariki ambazo ni Rwanda, Malawi, Zambia na Zombabwe .

Kwa upande wake, TIC ilipongeza juhudi kubwa zinazofanywa na wenye kiwanda hicho kuzalisha bidhaa bora ambazo zinawezi kushindana kwenye soko la kimataifa.

Meneja wa TIC Kanda ya Mashariki, Bevin Ngenzi alisema ameshangazwa na ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho ambazo mtu anaweza kudhani kwamba zinatoka nje ya nchi.

"'Tunawashukuru na kupongeza kwa kazi nzuri mnayofanya, mmeajiri Watanzania wengi sana na mnazalisha bidhaa ambazo kwa kweli tumeona ubora wake ni wa hali ya juu sana hongereni sana," alisema

# Mteja Exim kipaumbele huduma za kimtandao

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imesisitiza kuhusu mkakati wake wa kuwekeza na kutanguliza zaidi maslahi ya wateja wake hususani katika mipango yake muhimu ikiwemo ile ya uvumbuzi na utoaji wa huduma kwa wateja. Akizungumza kuhusiana na mkakati huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Jaffari Matundu, alisisitiza kuwa benki hiyo imejizatiti kuhakikisha kwamba wateja wake wananufaika zaidi na ukuaji wa technolojia katika utoaji wa huduma za kibenki.

"Lengo ni kuhakikisha kwamba benki ya Exim tunatumia vyema huu ukuaji wa kidigitali katika utoaji wa huduma za kibenki kwa wateja wetu…lengo ni kuona wanaridhishwa na huduma zetu na wanazifurahia. Tunaamini kwamba furaha na ukuaji wao ndio biashara yetu,'' alisema.

Aliongeza kuwa ajenda ya uvumbuzi imebaki kuwa kipaumbele cha benki hiyo katika kuelekea kwenye lengo lake la msingi ambalo ni kuifanya benki hiyo kuwa ya kidigitali zaidi huku kipaumbele kikibaki kuwa ni 'mteja kwanza'.

Katika kabiliana na changamoto ya COVID 19, benki hiyo mapema mwaka jana ilizindua kampeni ya "Maliza Kirahisi Kidigitali' iliyodumu katika kipindi cha mwaka mmoja ikilenga kubadilisha tabia ya wateja na kuongeza kasi ya mabadiliko yanayoendelea ya nchi kutoka katika kutumia pesa taslimu kwenda malipo ya dijiti.

"Kampeni hiyo pia inakwenda sambamba na kuunga mkono mkakati wa Serikali wa kuhamasisha matumizi ya kidigitali katika kufanya miamala uchumi pamoja na kuhakikisha wateja wetu wanahudumiwa bila kwenda kwenye matawi," aliongezea.

Ili kurahisisha zaidi miamala na kuifanya bora zaidi na rahisi kwa wateja, benki ina chaguzi kadhaa za huduma kupitia simu na kidigitali ambazo wateja wanaweza kuzitumia kupata huduma na kufanya miamala muda wowote katika siku saba za wiki. Katika kuhakikisha kwamba huduma za benki hiyo zinakuwa jumuishi, huduma ya USSD ndio ilihusika katika kuipamba kampeni hiyo.

''Kila mwingiliano na mteja ni nafasi kwetu kuwaelewa vizuri wateja wetu na namna ya kuwahudumia kulingana na mahitaji yao. Tunapoendelea kupanua huduma zetu, tunaweza kuona jinsi kila huduma inatimiza mahitaji ya watumiaji. Ni suala la kuendelea kujifunza na uvumbuzi. ''

Nipashe
# Spotika



WACHEZAJI KUMI WANAOLIPWA ZAIDI TOFAUTI NA KIWANGO CHAO UK. 12-13




# NYOTA WA5 VIWANGO WASIOPEWA NAFASI

## ISIKUPITE

TANGU Kocha Thomas Tuchel aanze kuinoa Chelsea kwa mara ya kwanza Januari, mwaka huu, 'Blues' hao wamecheza mechi nyingi zaidi bila kuruhusu bao 'clean sheets' (14) katika mashindano yote kuliko timu yoyote kwenye ligi bora tano kubwa Ulaya. Hadi sasa imepata clean sheets 14 katika mechi 19.



**LONDON,** England

KATIKA kikosi cha wachezaji 22 kuchagua 11 tu wa kucheza si kazi rahisi kwa kocha yeyote. Hata hivyo, lazima uamuzi ufanyike na wachezaji kadhaa hujikuta wakikosa nafasi ya kucheza. Katika klabu kubwa, ushindani wa namba ni mkubwa sana.

Mashabiki huwa wanapaza sauti zao kwenye mitandao ya kijamii wakati nyota wao wanapokosa nafasi ya kucheza.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao hawapati nafasi ya kucheza kwenye klabu zao kwa sasa, shuka nayo...

**#5. ISCO (REAL MADRID)**

Alikuwa akichukuliwa kama mmoja wa viungo washambuliaji bora kabisa duniani miaka michache iliyopita, lakini sasa Isco maji yamezidi unga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Real Madrid akitokea Malaga kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 27 mwaka 2013, akikataa ofa ya Manchester City. Isco alikuwa mchezaji muhimu wakati wa miaka yake ya kwanza pale Real Madrid.

Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni, Isco amekuwa akitumika kama mchezaji wa ziada pale Madrid. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, amecheza mechi 321 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo, akifunga mabao 51. Msimu huu amecheza mara 18 tu kwenye ligi, huku akianza mara sita. Hajafunga bao wala pasi ya mwisho.

**#4. MIRALEM PJANIC (BARCELONA)**

Usajili wa Miralem Pjanic pale Barcelona uliibua mjadala wakati akisajiliwa na hajapata muda wa kutosha kucheza.

Pjanic alifurahia wakati wake wa kucheza akiwa kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A kwenye klabu za AS Roma na Juventus. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Bosnia and Herzegovina, alihamia Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita, huku akipishana na Arthur aliyejiunga na Juventus.

Pjanic mwenye umri wa miaka 31, amecheza mechi 17 tu kwenye LaLiga msimu huu, sita akianza. Nafasi yake imekuwa ikichezwa zaidi na Sergio Busquets na Frenkie de Jong.

**#3. DELE ALLI (TOTTENHAM HOTSPUR)**

Wakati Jose Mourinho alipoteuliwa kuwa kocha wa Tottenham Hotspur, wengi waliamini kwamba, ujio huo utakuwa msaada mkubwa kwa kiwango cha Dele Alli.

Mourinho amekuwa akimtumia mara chache sana Alli, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Paris Saint-Germain. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amecheza mechi tisa tu za ligi msimu huu, akianza mara mbili.

Na nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, kuna uwezekano mkubwa akaondoka hapo Tottenham Hotspur kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Na uhamisho wa kwenda Paris Saint-Germain unaonekana kuwa na nafasi kubwa zaidi ili akaungane na kocha wake wa zamani, Mauricio Pochettino, ambaye aliyemjengea jina.

**#2. DONNY VAN DE BEEK (MANCHESTER UNITED)**

Donny van de Beek ambaye ni mhitimu wa akademi ya Ajax, alitua Manchester United kwa dau kubwa na amekuwa na mwanzo mgumu kwenye Ligi Kuu England.

Man United walilipa pauni milioni 35 kwa Ajax kwa ajili ya kupata huduma ya Van de Beek kipindi cha majira ya joto kilichopita. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alionekana kama angeleta ushindani mkubwa kwa Bruno Fernandes, lakini mambo yamekuwa tofauti kabisa.

Van de Beek amecheza mara chache sana msimu huu na nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi ameanza mara mbili tu kwenye ligi. Wengi wanaamini kwamba, iwapo Paul Pogba ataondoka hapo kuna uwezekano wa yeye kupata nafasi ya kutosha kucheza.

**#1. AYMERIC LAPORTE (MANCHESTER CITY)**

Alikuwa mmoja wa walinzi bora wa kati msimu mmoja uliopita, lakini sasa Aymeric Laporte ni chaguo la tatu pale Manchester City.

Uwapo wa John Stones na Ruben Dias, umemfanya Laporte kutopata nafasi ya kutosha kucheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye anaweza pia kucheza kama mlinzi wa kushoto, ameanza mechi 12 kwenye Ligi Kuu England kwa Manchester City msimu huu.

Huku kocha Pep Guardiola akiwa anapenda zaidi kuwatumia Stones na Dias kwenye safu ya ulinzi wa kati, ni wazi kwamba, nafasi ya Laporte kucheza ni finyu sana.

Mfaransa huyo aligharimu Man City pauni milioni 57 wakati alipojiunga nayo akitokea Athletic Bilbao Januari mwaka 2018.

## Extra Time

# WACHEZAJI KUMI WANAOLIPWA ZAIDI TOFAUTI NA KIWANGO CHAO

**LONDON,** England

MPIRA wa miguu ni moja ya michezo inayotazamwa zaidi duniani, na unaingiza kiwango kikubwa cha fedha. Moja ya wanamichezo wanaolipwa zaidi duniani ni wachezaji wa mpira wa miguu, akiwamo nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo na Lionel Messi wa Barcelona.

**Baadhi ya klabu kubwa duniani, ikiwamo Manchester United, Real Madrid na Barcelona, zina bajeti kubwa zaidi ya mishahara.**

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 ambao wanalipwa mishahara mikubwa zaidi tofauti na viwango vyao vya sasa dimbani, twenda sasa...

### #10. SAMUEL UMTITI (BARCELONA) – PAUNI 208,000 KWA WIKI

Msimu wake wa kwanza Samuel Umtiti pale Barcelona ulikuwa wa furaha kubwa kwa mashabiki wa klabu hiyo na wakiamini ndio mrithi sahihi wa Gerard Pique.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alijiunga na Barcelona akitokea Lyon mwaka 2016 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 22.5 na haraka alionyesha kiwango cha kuvutia kama mlinzi wa kati. Hata hivyo, misimu iliyofuata haikuwa mizuri kwake, huku akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na hivyo kuwafanya Clement Lenglet na Oscar Mingueza kuchukua nafasi yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amecheza mechi 129 kwenye mashindano yote ndani ya klabu hiyo.

### #9. JUAN MATA (MANCHESTER UNITED) – PAUNI 150,000 KWA WIKI

Juan Mata alikuwa mmoja wa viungo washambuliaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu England wakati akiwa kwenye ubora wake, lakini siku hizi hana kabisa nafasi ya kucheza pale Manchester United.

Wakati Man United walipomsajili Mata kutoka Chelsea Januari 2014, kwa ada iliyoweka rekodi kipindi hicho ya pauni milioni 40, kulikuwa na matarajio mengi kutoka kwake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa kikosi cha Chelsea kabla ya ujio wa Jose Mourinho.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, alifurahia wakati mzuri pale Man United wakati alipotua. Mata amecheza mechi 267 kwenye mashindano yote kwa 'Mashetani Wekundu' hao akifunga mabao 50 na kutoa pasi za mwisho 47.

### #8. MAURO ICARDI (PARIS SAINT-GERMAIN) – PAUNI 168,000 KWA WIKI

Mauro Icardi ni mshambuliaji mwenye kipaji, lakini nje ya dimba amekuwa mtata sana pale Paris Saint-Germain.

Wakati akiwa kule Inter Milan raia huyo wa Argentina alionekana angekuwa gwiji wa klabu hiyo. Licha ya rekodi yake nzuri ya kufunga mabao, uhusiano yake mabovu na mashabiki yakamfanya asipendwe na akapelekwa kwa mkopo Paris Saint-Germain mwaka 2019.

Miamba hao wa Ligue 1 waliamua kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa mkataba wa kudumu mwaka 2020, kwa ada ya pauni milioni 45. Msimu huu Icardi hajatumiwa sana. Ujio wa Moise Kean, pamoja na uwapo wa nyota Neymar, Kylian Mbappe na Angel Di Maria, umemfanya Icardi kucheza mechi 19 tu kwenye mashindano yote msimu huu, huku akifunga mabao saba.

### #7. AARON RAMSEY (JUVENTUS) – PAUNI 250,000 KWA WIKI

Mshahara wa Aaron Ramsey ulikuwa majadala mkubwa wakati alipojiunga na Juventus. Ramsey mara zote alikuwa anataka mshahara mkubwa, hasa ukizingatia kwamba, alijiunga na Juventus akiwa mchezaji huru. Raia huyo wa Wales alikuwa na kiwango cha kuvutia zaidi wakati akicheza Arsenal, lakini sasa hapati kabisa nafasi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, aliamua kujiunga na Juventus mwaka 2019, hajawa katika ubora wake. Ramsey amecheza mechi 62 kwenye mashindano yote akifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho sita. Kumekuwa na uvumi kwamba Juventus wanaweza kumuachia aondoke kipindi cha majira ya joto wakati wakipanga kukisuka upya kikosi chao. Arsenal, Manchester United na Tottenham Hotspur zimehusishwa naye.



JUAN MATA

### #6. EDEN HAZARD (REAL MADRID) – PAUNI 416,000 KWA WIKI

Eden Hazard alikuwa anatajwa kama mrithi sahihi wa Cristiano Ronaldo wakati anajiunga na Real Madrid. Lakini ni ukweli ulio wazi kwamba, uhamisho huo haukuzaa matunda kama ilivyotarajiwa.

Hazard aliondoka Chelsea mwaka 2019, na kujiunga na Real Madrid kwa ada ya uhamisho wa pauni 103.5. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, alikuwa akitajwa kama mmoja wa wachezaji bora duniani wakati aliposajiliwa hapo Real Madrid na kupewa jezi namba saba.

Mi misimu miwili sasa imepita, na Hazard hajawa na muda wa kutosha kucheza pale Real Madrid. Majeraha ya mara kwa mara yamemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, kutopata nafasi ya kucheza. Hazard amecheza mechi 36 katika mashindano yote tangu atue hapo, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho saba.

### #5. PAUL POGBA (MANCHESTER UNITED) – PAUNI 300,000 KWA WIKI

Moja wa viungo bora Ulaya wakati alipokuwa kwenye ubora wake, lakini sasa Paul Pogba amekuwa na wakati usiovutia pale Manchester United.

Ni zao la akademi ya Man United na Pogba alijiunga tena na timu hiyo mwaka 2016 akitokea Juventus kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 94.5. Tangu hapo kumekuwa na wakati usiovutia. Mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Old Trafford.

Mchezaji huyo kwa sasa hana nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi hicho na kuna uwezekano mkubwa akaondoka mwishoni mwa msimu huu.

### #4. KEPA ARRIZABALAGA (CHELSEA)- PAUNI 180,000 KWA WIKI

Wakati unapokuwa golikipa ghali zaidi duniani, unatarajiwa kuanza katika kila mchezo, lakini mambo ni tofauti kwa Kepa Arrizabalaga.

Chelsea ililipa pauni milioni 72 kwa Athletic Bilbao kwa ajili ya kumchukua kipa huyo mwenye umri wa miaka 26, mwaka 2018 kuziba nafasi ya Thibaut Courtois, lakini amekuwa chaguo la pili mbele ya Edouard Mendy aliyesajiliwa kipindi cha majira ya joto kilichopita. Msimu huu amecheza mechi tisa tu na Valencia imekuwa ikihusishwa naye.

### #3. GARETH BALE (TOTTENHAM HOTSPUR, REAL MADRID)- PAUNI 600,000 KWA WIKI

Mmoja wa wachezaji bora duniani wakati akiwa kwenye ubora wake, Gareth Bale na ameendelea kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi duniani.

Baada ya kushindwa kupata nafasi kule Real Madrid, Bale alirudi Tottenham Hotspur kwa mkopo kipindi cha majira ya joto kilichopita. Nyota huyo wa kimataifa wa Wales ambaye alikuwa mchezaji ghali zaidi wakati alipojiunga na Real Madrid, hana nafasi kikosi cha kwanza chini ya kocha, Jose Mourinho msimu huu.

Bale amecheza mechi 26 kwenye mashindano yote kwa Spurs msimu huu, akifunga mabao 10 na kutoa pasi tatu za mwisho.

### #2. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG (ARSENAL) – PAUNI 350,000 KWA WIKI

Wakati Arsenal walipokuwa wanampa mkataba mpya Pierre-Emerick Aubameyang kipindi cha majira ya joto kilichopita, straika huyo alikuwa mchezaji muhimu sana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon, amefunga mabao 29 katika mechi 44 kwenye mashindano yote msimu uliopita, na mkataba mpya ulionekana kuwa muhimu.

Lakini msimu huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amekuwa na wakati mgumu, akicheza mechi 33 kwenye mashindano yote na kufunga mabao 14.

### #1. DAVID DE GEA (MANCHESTER UNITED) – PAUNI 350,000 KWA WIKI

Mmoja wa magolikipa bora katika kizazi cha sasa, lakini muda wa David de Gea pale Manchester United unaonekana kuelekea ukingoni. Uwapo wa Dean Henderson umefanya majaliwa ya de Gea kuwa shakani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, amekuwa hana nafasi kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

De Gea mwenye umri wa miaka 30, amecheza mechi 435 katika mashindano yote kwa klabu hiyo tangu alipojiunga nayo mwaka 2011. Amekuwa akihusishwa na Paris Saint-Germain, na Man United wanaweza kumuachia aondoke.

## Nukuu

"Alinifundisha kuhusu njia ya 'kuwa Mfaransa'... alinielezea namna ya kuwa Mfaransa, namshukuru sana kwa kunisaidia kuzoea maisha ya hapa, na hivyo furaha yangu ipo hapa, nilifurahi sana kukutana na huyu mtu hapa. Kylian ni mtu mwenye utu sana, mara zote ana furaha na ana adabu kwa kila mtu," **mshambuliaji wa PSG, Neymar akimshukuru Kylian Mbappe.**



"Anajua hisia zangu; najua hisia zake. Bado hajafikia uamuzi. Naelewa umekuwa mwaka mgumu kwa kila mtu, lakini kwa mtu mpya ambaye hazungumzi Kiingereza, hana tamaduni za Uingereza, kuona watu wakiwa na marafiki zao na yeye hana ni jambo gumu kwake, nimefunga vidole vyangu, naamini anaweza kubaki baada ya msimu huu, tumekuwa na bahati naye nzuri," **Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, akionyesha matumaini ya kumshawishi Edinson Cavani kubaki Old Trafford.**



"Moja ya sababu ni kukosekana kwa mashabiki wetu, hakuna shaka na hilo, timu nyingi zina tatizo hilo. Mbali na sababu hiyo kwa nini hatushindi mechi zetu za nyumbani ni kwa sababu hatuchezi vizuri. Kuna baadhi ya mechi za nyumbani tulizopoteza ambazo nafikiri hata bila mashabiki tulipaswa kushinda kwa uhakika kabisa, lakini hatukushinda," **Kocha wa Liverpoo, Jurgen Klopp akililia mashabiki Uwanja wa Anfield**





Straika wa Yanga, Yacouba Sogne, akishangilia bao pekee lililowapa ushindi wa 1-0 dhidi ya Biashara United huku Tuisila Kisinda akimfuata kumpongeza. Mechi hiyo ilichezwa Jumamosi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI TANO KALI LIGI KUU BARA IKIYOYOMA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walipata ushindi wa mabao 5-0 Jumatano iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar, huku Yanga ikishinda kwa bao 1-0 Jumamosi usiku dhidi ya Biashara United, mechi zote zikipigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Ligi hiyo, iliendelea Aprili 8, mwaka huu baada ya kusimama kwa muda wa mwezi mzima, kupisha michuano ya kufuzu kwa Fainali za Mataifa ya Afrika, pamoja na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk, John Magufuli.**

Ipo kwenye raundi ya 26 kwa baadhi ya timu, zingine 25, kuna zilizocheza mechi 24, Simba ikicheza mechi 21 sawa na na Namungo kabla ya mechi za jana. Tangu ligi irejee, kumekuwa na rekodi mbalimbali zikiwekwa na timu pamoja na wachezaji.

Makala haya yamekusanya rekodi mbalimbali zilizowekwa tangu ligi hiyo iliporejea tena, twende sasa...

**#1. YANGA KUSHINDA BAADA YA MECHI TATU**

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata Yanga dhidi ya Biashara United Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa umekuwa wa kwanza baada ya mechi tatu za ukame kupita. Kabla ya mechi hiyo, mara ya mwisho Yanga kushinda ilikuwa Februari 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ilipoichapa Mtibwa Sugar bao 1-0.

Baada ya hapo Machi 4 ilikwenda Uwanja wa Mkwakwani Tanga na kupata kipigo cha mabao 2-1 kisha Machi 7 ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha na Aprili 10 ikazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC.

**#2. SIMBA UGENINI TANGU FEBRUARI**

Simba ilicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ugenini tangu Februari mwaka huu. Mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Mwandui kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga jana Jumapili, ilikuwa ni ya kwanza tangu Februari 18 ilipocheza karika Uwanja wa Karume mjini Musoma, mkoani Mara.

Ni mechi ambayo Simba ilitoka uwanjani na ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Benard Morrison. Tokea hapo timu hiyo haikucheza tena mechi yoyote ya ligi ikiwa ugenini zaidi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku pia ikiendelea na mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

**#3. BIASHARA BILA BARAZA MAJANGA**

Tangu kuondoka kwa Kocha Mkuu Francis Baraza, Biashara haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara. Baraza, raia wa Kenya ambaye aliifanya Biashara United kuwa tishio, alitimka kwenye timu hiyo na kwenda Kagera Sugar.

Kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga Jumamosi iliyopita ni mwendelezo wa matokeo mabovu tangu kuondoka kwake. Mechi ya kwanza ambayo Biashara United ilicheza bila Baraza ni ya Aprili 9, mwaka huu ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania, kabla ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union na imetimiza mechi ya tatu kutoshinda kwenye mechi hiyo dhidi ya Yanga.

**#4. GWAMBINA HOI MECHI YA TANO**

Baada ya kutopoteza mechi yoyote ile kwenye michezo yake minne ya Ligi Kuu, hatimaye Gwambina FC ilikiona cha moto ilipochapwa mabao 3-0 Ijumaa iliyopita dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ni kipigo kizito, hasa ikizingatia kuwa ilikuwa na mfululizo wa matokeo mazuri ya kucheza mechi nne mfululizo bila kupoteza. Mara ya mwisho ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting Februari 16, lakini kuanzia hapo iliichapa Ihefu mabao 2-1 Machi 3, kisha Machi 7 ikamfumua Mtibwa Sugar mabao 2-0, huku Machi 13 ikitoka suluhu dhidi ya Polisi Tanzania na Aprili 10, mwaka huu ikaishindilia Coastal Union mabao 4-0, kabla ya kukutana na kipigo kutoka kwa KMC.

**#5. KAGERE KURUDI KILELENI**

Ni wiki iliyoshuhudia mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwa misimu miwili mfululizo kwenye Ligi Kuu, Meddie Kagere, akirejea tena kileleni baada ya kupachika mabao mawili katika ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumatano iliyopita.

Kagere msimu huu amekuwa hapati sana nafasi ya kucheza, lakini amekuwa akionyesha umahiri wake wa kupachika mabao kila anapopata nafasi ndogo dimbani.

Mnyarwanda huyo ambaye anawania ufungaji bora mara ya tatu mfululizo kuweka rekodi ya kihistoria kwenye Ligi ya Tanzania kwani tangu ianzishwe mwaka 1965, hakuna mchezaji yeyote iwe wa Kitanzania au nje nchi aliyeibuka mfungaji bora mara tatu mfululizo.

Kabla ya mechi ya jana dhidi ya Mwadui FC, Kagere tayari alikuwa na mabao 11, akiwa juu ya Mzimbabwe Prince Dube wa Azam FC ambaye ana mabao 10 mpaka sasa.

**JE, WAJUA?**



ZIKIWA zimebaki mechi sita kabla ya kumalizika kwa Ligi Kuu England, Sheffield United imekuwa miongoni mwa timu zilizowahi zaidi kushuka daraja katika historia ya ligi hiyo ikiungana na Ipswich Town msimu wa 1994-95, Derby County (2007-08) na Huddersfield Town (2018-19).



# OSHA yatathmini matukio ya ajali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), umeagizwa kufanya tathmini ya maeneo ya kazi yanayoongoza kwa matukio ya ajali na magonjwa.

Pia wakala huo utabainisha visababishi vyake ili kuwezesha uandaaji wa mkakati wa kudhibiti visababishi hivyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alitoa agizo hilo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua kikao cha pili cha baraza la wafanyakazi wa OSHA lenye lengo la kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwamo kuondoa baadhi ya tozo ambazo zilionekana kuwa kero, hivyo nawaagiza kuendelea kufanya kazi kwa weledi na uadilifu ili kufikia lengo letu la kupunguza ajali na magonjwa yatokanayo na kazi na kuleta ustawi wa Taifa letu," alisema Mhagama.

Alishauri wajumbe wa kikao hicho kufanya majadiliano katika kikao hicho kwa hekima na busara na hatimaye kutoka na maazimio muhimu ambayo yatafanyiwa kazi ili kutimizi malengo ya taasisi.

Aidha, aliitaka OSHA kuendelea kubuni mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo itaboresha utoaji wa huduma kwa wadau pamoja na kuweka taratibu za huduma ambazo ni rafiki kwa wadau ili kuendana na maelekezo ya serikali.

Awali, Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema maboresho ambayo yamekuwa yakifanyika na serikali katika sekta ya biashara na uwekezaji ikiwamo kuondoa baadhi ya tozo, yamepelekea taasisi hiyo kupata mafanikio makubwa ikiwamo kuongeza usajili wa maeneo ya kazi kutoka 5,300 hadi 20,000 kwa kipindi kati ya mwaka wa fedha 2014/2015 na 2020/2021.

Kwa upande wao, mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) Taifa, Fidelis Athuman na Mjumbe wa Baraza hilo, Joyce Mwambungu, walipongeza serikali na uongozi wa OSHA kwa maboresho ya utendaji ambayo yamekuwa yakifanyika kutokana na ushirikishwaji wa watumishi kupitia vikao vya mara kwa mara vya baraza la wafanyakazi.



Katibu wa Mradi wa Majitaka wa Mtaa wa Kinyambwa Road, Kata ya Kikuyu Jiji la Dodoma, Peter Ishebabi, akiwaonyesha baadhi ya wakazi wa mtaa huo ramani ya miundombinu ya uwekaji wa mabomba yatakayotolewa na Mamlaka ya Maji safi na Majitaka na Usafi wa Mazingira (DUWASA), ambayo hadi kukamilika kwake utakagharimu Sh. milioni 270.5. **PICHA:PETER MKWAVILA.**

# Wauza matunda, mboga waonyeshwa fursa sokoni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara wa mboga na matunda kuchangamkia fursa iliyopo kwenye soko la Ndugai ambalo limetenga eneo kwa ajili yao.

Aidha, amesema kuwa serikali haikulijenga soko hilo kwa lengo la kutaka kuyabomoa masoko yaliyopo ndani ya Jiji hilo, bali imepanua wigo wa wananchi kupata huduma. Yuna aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu taarifa zinazotolewa na baadhi ya viongozi wa masoko, kudai kuwa serikali imelijenga soko hilo kwa ajili ya kuwahamisha wafanyabiashara na kuyabomoa masoko yaliyopo.

Alisema Jiji hilo kutokana na ongezeko la watu maeneo mbalimbali limefanya jitihada za kusogeza huduma ya masoko kwenye maeneo yao.

"Ninaomba nisisitize hapa kwa wafanyabiashara wote ndani ya masoko yaliyopo jijini hapa,kuwa serikali halijalijenga soko la Ndugai ili kuvunja masoko mengine bali limeongeza huduma kwa wananchi wote, pia jiji halitawahamisha wafanyabiashara kwenye masoko yao hivyo kwa wale watakaokuwa tayari kwenda nawaomba wachangamkie fursa hiyo," alisema.

Akizungumza na wafanyabiashara wa soko la mboga na matunda Makole, Yuna alisema Jiji tayari limeshatenga maeneo mbalimbali kwa makundi na haina mpango wa kuvunja soko hilo.

Nao, wafanyabiashara wa soko la Makole walisema walikumbwa na taharuki baada ya kusikia taarifa kuwa soko hilo litabomolewa na wao kuhamishiwa soko la Ndugai.

# Washauriwa kuwaepuka ulipaji kodi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imewashauri wafanyabiashara kulipa kodi yao kwa mujibu wa taratibu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuepuka matapeli wanaopiga simu kuwapa vitisho.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malalamiko wanayopata kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara na watumishi wa umma, ambao wametapeliwa na watu hao.

"Unakuta baadhi ya wafanyabiashara na watumishi wa umma kutoka mikoa mbalimbali wanapigiwa simu na watu wanaojifanya ni maofisa TAKUKURU Dodoma kuwaita waje, huku wakiwatishia ya kuwa wanamakosa kadhaa ikiwemo kuwaomba rushwa, lakini wakifika wanakuta hakuna Ofisa yoyote wa TAKUKURU aliyewaita."

"Nawaomba wafanya biashara na watumishi wa umma kuweni makini na suala hili watu wanaofanya hivyo ni matapeli na TAKUKURU haitoi huduma kwa gharama yoyote ya pesa hivyo ukiona umepigiwa simu na mtu anayejifanya ni Ofisa wa TAKUKURU kutoa taarifa kupitia namba ya simu ya taasisi hiyo," alisema.

Alisema mtu akiwa mkoa mwingine akaambiwa unaitwa Dodoma na TAKUKURU basi ni vema akajiridhisha kupitia ofisi zake zilizopo mkoa anaotoka ili kuepuka kutapeliwa.

"Unakuta wanawapigia wafanyabiashara na watumishi kuwaita Dodoma, wakijitambulisha wao ni maofisa TAKUKURU wakifika huku wanakuta hakuna aliyewaitwa na kuishiwa kutapeliwa," alisema Kibwengo.

Aidha, aliwahimiza wafanyabiashara, watumishi na jamii kwa ujumla kufanya kazi zao kwa weledi ikiwamo kulipa kodi ya mapato kama unatakiwa.






Mtendaji Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Empower Society Transform Lives (ESTL), Joshua Lissu, akizungumza katika kikao kazi cha Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto ngazi ya mkoa (MTAKUWWA) kilichoketi mwishoni mwa wiki. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Walimu wakuu wafundwa ufaulu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MTENDAJI Mkuu wa Taasisi ya Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu nchini (ADEM), Dk. SISTON Masanja, amewataka walimu wakuu 210 waliopata mafunzo ya udhibiti ubora wa shule wa ndani kutoka mkoani Songwe kuyatumia vyema mafunzo waliyoyapata ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Dk. Masanja aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kuhitimisha mafunzo ya siku tatu kwa walimu wakuu wa shule kutoka mkoani Songwe yaliyofanyika jijini Mbeya katika Kituo cha mafunzo ADEM, Kampasi ya Mbeya.

Alisema mafunzo hayo yana lengo la kudhibiti ubora wa shule, ubora wa mtaala katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi, ubora wa ufundishaji kwa ujifunzaji na upimaji mzuri, mafanikio ya mwanafunzi katika taaluma, ubora wa uongozi na utawala wa shule, ushirikishwaji wa jamii katika udhibiti ubora wa shule.

Alisema vipengele hivyo nane vina lengo la kuboresha na kuinua kiwango cha elimu wa shule zote mkoani Songwe, na kwamba baada ya mafunzo hayo wanatarajia kuona mabadiliko.

"Mafunzo haya yamewaongezea umahiri katika uongozi, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa maelekezo ya serikali kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu ili kuleta matokeo chanya na kuboresha utendaji kazi," alisema Dk. Masanja.

Alisema wanatarajia washiriki kutumia umahiri, mbinu, maarifa na ujuzi waliopata kuboresha na kusimamia shule zao kwa umahiri mkubwa ili elimu bora itolewe kwa wanafunzi na Watanzania kwa ujumla.

Aliwasisitiza walimu hao kuweka ratiba ya ufuatiliaji na tathmini kwa kuyaeleza yote wanayoyatekeleza katika kazi zao lengo likiwa ni kuboresha na kuongeza kazi ya utendaji kazi.

Aidha alizishauri kamati za shule kuhamasisha wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao ili kuinua kiwango cha ufaulu lakini pia ushirikishwaji wa jamii katika uthibiti ubora wa shule.

Mratibu wa Mafunzo ADEM, Kampasi ya Mbeya, Petro Wawa, alisema watahakikisha wanaimarisha ukaguzi wa shule kwa ili elimu kuwa bora mkoani Songwe.

Alisema licha ya walimu 210 kunufaika na mafunzo hayo, lakini bado kuna uhitaji wa mafunzo hayo shule nyingine ambazo ni mpya.

Alieleza jumla ya shule 25 ambazo ni mpya walimu wakuu wake hawajapata mafunzo, hivyo wanaandaa utaratibu wa namna wapate elimu hiyo.

"Washiriki 43 wametoka Ileje, Halmashauri ya Momba, 33, Mbozi 88, Songwe 26 na Tunduma 20, nawashauri elimu mliyoipata mkaitoe na kwa walimu wenzetu ili kuboresha utendaji kazi wenu," alisema Wawa.

Flavian Mmbaga, Meneja ADEM Kampasi ya Mbeya, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha mazingira ya kusoma na kujisomea ili kuendana na viwango vya kimataifa vya utoaji elimu.

Aliongeza kuwa thamani ya fedha inayotumika kujenga miundombinu ya shule inaendane na majengo yaliyopo ikiwa ni sehemu ya udhibiti ubora wa shule ubora wa mazingira, ustawi na elimu ya majanga shuleni.

# Mwanaharakati aja juu ya JPM kubezwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWANAHARAKATI na mchambuzi wa siasa jijini Mbeya, John Nswila, amewataka wanasiasa kuacha unafiki wa kubeza shughuli za maendeleo zilizofanywa na Hayati Dk. John Magufuli.

Nswila aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wanahabari juu ya maoni aliyonayo kuhusu baadhi ya watu wanaobeza kazi alizozifanya Hayati. Dk. Magufuli.

Alitoa rai kwa wanasiasa kuacha tabia ya ukigeugeu badala ya kumsifia hayati Dk. Magufuli enzi za uhai wake, lakini sasa wanakosoa mambo ambayo aliyafanya akitolea mfano wa hasara iliyopatikana kwenye uendeshaji wa Shirika la Ndege (ATCL) na miradi mingine ambayo ilikuwa ikitekelezwa kipindi hicho.

Aliongeza kuwa baadhi ya wanasiasa hususani wabunge wamekuwa wakifanya mambo kwa maslahi yao binafsi wakishindwa kuwa wakweli na kuweka mbele tamaa zao za kupata madaraka na kusahau jukumu lao la kuwatumikia wananchi .

Hata hivyo alimshauri Rais Samia Suluhu Hassan kuwa makini na wanasiasa wanafiki, wanaomsifia ili kupata madaraka bila kujali maslahi mapana ya Taifa.

"Nachukizwa na baadhi ya wanasiasa nchini ambao wanamkejeli Hayati Dk. Magufuli wakidai hajafanya chochote cha maana kwa Watanzania au alikuwa anapendelea baadhi ya wachache... lengo lao likiwa ni kujitengenezea mazingira rahisi ya kushinda uchaguzi wa mwaka 2025, hao ndio wachawi wa taifa kwa sababu wanamkwamisha Rais Samia katika kuwatumikia wananchi kikamilifu," alisema Nswila.

Aidha, aliwaomba wanasiasa wastaafu kutotumia mitandao ya kijamii kama sehemu ya kutoa ushauri kwa Rais hasa kwa mambo muhimu yanayohusu mustakabali wa taifa, badala yake wazungumze naye Rais moja kwa moja.

# Mfuko wa jimbo watoa mil. 58/- vifaa vya ujenzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya imetoa vifaa vyenye thamani ya Sh.milioni 58 vya ujenzi kutoka kwenye mfuko wa jimbo.

Imeelezwa kwamba lengo ni kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imeibuliwa na wananchi.

Akizungumza jana, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Filbert Mbwilo, alisema kuwa fedha hizo zimetumika kununua vifaa mbalimbali vya ujenzi ikiwamo bati, saruji pamoja na nondo na kwamba vitaelekezwa kwenye zahanati, shule na vituo vya afya.

Alitaja maeneo ambayo yatanufaika na fedha hizo ni Kata ya Santilya, Mshewe, Ijombe, Igoma, pamoja na Igale yataongezewa nguvu baada ya wao kuibua miradi mbalimbali na kuanza kuitekeleza.

"Fedha za mfuko wa jimbo zinatolewa kwa ajili ya kuchochea shughuli za maendeleo ambazo tayari zimeanzishwa na wananchi katika maeneo na inapobidi mfuko huo huanzisha miradi mipya, tunaendelea kuwasisitiza wananchi waendelee kuanzisha miradi ya maendeleo serikali itakuja kuwaunga mkono," alisema Mbwilo.

Hata hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Steven Katemba, alisema kuwa fedha za mfuko wa jimbo hazitatolewa kwa wananchi ambao hawajitolea kufanya shughuli yeyote ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zitapelekwa sehemu ambayo tayari wananchi wameanzisha mradi na kwamba Halmashauri nayo kupitia mapato yake ya ndani itawasaidia.

Katika hatua nyingine Katemba alisema Halmashauri imetoa mikopo ya zaidi ya Sh.milioni 200 kwa vikundi 15 vya wanawake, vijana na walemavu.

Alisema mbali na kutoa mikopo ya fedha kwenye baadhi ya vikundi pia wametoa vifaa kama mashine pamoja na pikipiki ili kuwawezesha wananchi kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao yao na kurejesha mikopo kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwataka wananchi walionufaika na mikopo hiyo kuhakikisha wanarejesha kwa wakati ili na wengine waweze kunufaika na mikopo hiyo.

# 'Z'bar yafungia pombe hadi Ramadhani iishe'

**Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BODI ya Vileo Zanzibar, imefunga maduka ya jumla na ya wakala wa vileo na kukataza unywaji kupisha Mfungo wa Ramadhani.

Kutokana na hatua hiyo, uhaba wa vileo umejitokeza katika hoteli za kitalii na kwenye maeneo ya burudani zinazohudumia watalii katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI) Taleeb Jussab, alisema , hatua hiyo imesababisha malalamiko kutoka kwa wanachama wao kuhusu kuadimika kwa vileo baada ya maduka kufungwa.

Alisema bodi hiyo imefunga maduka ya vileo bila ya kuwashirikisha wadau katika sekta ya utalii na kusababisha usumbufu mkubwa kujitokeza katika upatikanaji wake mahotelini.

Jussab alisema pamoja na ZATI kuwa na mjumbe mmoja katika bodi lakini mpaka maduka ya vileo yanafikia kufungwa walikuwa hawana taarifa.

"Tumeanza kupokea malalamiko kutoka kwa wanachama wetu baada ya maduka kufungwa kuanzia April 15."alisema Jussab.

Hata hivyo, Katibu wa bodi hiyo, Zainab Makame Mussa, alisema sheria mpya ya vileo namba 9 kifungu cha 25(3), inaelekeza kuwa maduka ya wakala wa usambazaji vileo yanatakiwa kufungwa kupisha Mwezi wa Ramadhani.

"Bodi kazi yetu ni kusimamia sheria na kifungu cha 25(3)(4) kinazuia wamiliki wa maduka ya vileo kutoa huduma isipokuwa hoteli na migahawa ya kitalii,"alisema Zainab

Aidha, alikiri bodi ya vileo imetoa vibali kwa kampuni nane za kuingiza vileo badala ya tatu kinyume na kifungu cha 33(1) cha sheria ya vileo namba 9 ya mwaka 2020 kwa madhumuni ya kulinda mapato ya serikali.

Alisema kifungu cha 33 (1) cha sheria hiyo kinasema kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu kwa masharti wawe Wazanzibari, walipa kodi, wawe na ghala na magari ya kusambazia bidhaa.

Akizungumzia sakata hilo Mkurugenzi wa kampuni ya usambazaji vileo ya Scoch, Arvind Chandulal Asawla, alisema hoteli za kitalii zimekwama kupata huduma ya vileo baada ya wamiliki wa maduka kutakiwa kufunga huduma hiyo mpaka Mfungo wa Ramadhani utakapomalizika.

"Tunaomba serikali kuangalia , kwani kuna tatizo lililojitokeza kwa manufaa ya nchi na maendeleo ya sekta ya utalii kwa sababu ndio nguzo ya uchumi wa Zanzibar," alisema Asawlal wakati akizungumza na wanahabari.

Magari ya kubeba vileo kutoka katika mahoteli ya kitalii yamekuwa yakifika mjini na kulazimika kurudi bila ya vileo tangu kufungwa maduka wakati watalii wanahitaji huduma hiyo.



Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Juma, Ali Simai, akitoa taarifa ya Idara yake kwa Makamu wa Kwanza wa Rais. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# Mazingira wezeshi kunufaisha Watanzania uvuvi bahari kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Emanuel Andrew, amesema kuanza kutumika sheria mpya na kanuni za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kutaongeza uwekezaji kwa wazawa.

Aliyasema hayo katika mkutano wa wadau wakiwamo wanabahari na kuongeza kuwa kanuni zake zinalenga kuchochea uwekezaji katika uchumi wa bluu hasa kwa wazawa ili kuiendeleza sekta hiyo, kwani zipo nchi nyingi zimefanikiwa kutokana na kujiendesha kwa uvuvi na utalii.

Alisema ili kufikia lengo hilo katika utungaji wa sheria, serikali imetoa vivutio kwa wazawa hasa kwa vitu ambavyo vinahitaji gharama kubwa ikiwamo vifaa vinavyoingizwa kwa ajili ya uvuvi, kupunguza ada ya leseni na vifaa vyengine.

Alibainisha kuwa wazawa wanaweza kufaidika na uvuvi wa bahari kuu iwapo sekta binafsi zitawekeza katika eneo hilo na kupata faida ikiwemo ajira, chakula na viwanda kukua.

"Wavuvi wetu wadogo hawana uwezo wa kuvua bahari kuu na badala yake maji yetu yanavuliwa na meli za nje na kusababisha Tanzania isifaidike," alibainisha.

Aidha, alisema Tanzania ilikuwa inapata chini ya asilimia 10 ya faida katika uvuvi wa bahari kuu hivyo kupitia sheria hiyo mapato ya nchi yanaweza kukua kutokana na uvuvi huo.

Alisema ni wakati wa wavuvi kutumia fursa hiyo kwa kuvua katika bahari kuu ili kufaidika na sekta hiyo kwani uchumi wa bluu una faida kubwa.

"Sekta hii ina faida nyingi ikiwamo ajira na kukuwa kwa nyororo wa thamani sasa ni wakati kwa wazawa kuitumia fursa hii," alibainisha.

Alisema Zanzibar imeshaingia mkataba ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mpigaduri Unguja na Mkoani kisiwani Pemba.

Akiwasilisha mada ya sheria na kanuni za mamlaka Ofisa Sheria wa Mamlaka, Keis Issa Abdallah, alisema sheria hiyo imezingatia mambo mbalimbali ikiwamo uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali katika ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania (EEZ).

Aidha, alisema mambo mengine ni kuongeza wigo wa mipaka ya usimamizi wa meli zenye kupeperusha bendera ya Tanzania na kuzingatia mikataba na miongozo ya kikanda na ya kimataifa ya usimamizi wa ukanda wa uchumi wa bahari na rasilimali za uvuvi zinazopatikana baharini.

Alisema kifungu cha 45 na kanuni 47 vya sheria hiyo vimetoa fursa kwa mwekezaji mzawa au kampuni ya Tanzania inayomiliki zaidi ya asilimia 51 na mzawa kuomba vivutio kupitia mamlaka.

# Makamu wa Rais ataka ushirikiano

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, amewahimiza watendaji wa ofisi yake kushirikiana kutekeleza majukumu ili kufikia ufanisi.

Aliyaeleza hayo alipokutana na watendaji wakuu na wakuu wa vitengo na divisheni wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi , Idara ya Mipango Sera na Utafiti.

Aliwataka kushirikiana na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili kuwa na msimamo na uamuzi ya pamoja kwa kila hatua.

Aliwakumbusha watendaji kuwa wabunifu ili watakapoondoka waache kumbukumbu za kudumu kwenye taasisi na waliowaogoza .

Aliwafahamisha kuwa katika kuongoza wafanyakazi kiongozi lazima afahamu sheria za utumishi ikiwamo mfanyakazi anapofanya vizuri kuzawadiwa na kuwapa heshima yao kwani haki na wajibu ni mambo yanayo kwenda sambamba hasa katika utendaji.

Alisema viongozi wanatakiwa kusimamia sheria na taratibu hivyo, wafanyakazi wapewe heshima yao, kusimamiwa haki zao, wajibu wao wa kufanya kazi na kupewa maslahi yao kwa wakati ambayo wanastahiki jambo ambalo limeondoka katika utamaduni wa kufanya kazi.

'Imeshakuwa ni mazoea na tabia ya kuwafanya watumishi wa serikali ni watumwa wa serikali ni muhimu haki ifuatane na wajibu hata kama ni kidogo' alisisitiza Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kuhusu utendaji aliwaagiza viongozi kuona kila mfanyakazi anawajibika na kufahamu majukumu yake ya kwani mabadiliko hayawezi kutokea bila ya kuwapo uwajibikaji na kuwataka kuacha kufanya kazi kwa mazoea bali waendane na kasi ya mabadiliko ya utendaji. 'Mfanyakazi usisubiri kuulizwa jambo la kiutendaji limefikia wapi? Wakati unafahamu kuwa ili kazi ziendelee ni wajibu wako kutekeleza majukumu yako pamoja na kuwa mbunifu katika kazi zenu'

Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Khadija Khamis Rajab, aliwaomba watendaji na wakuu wa vitengo kuhakikisha maelezo yaliyotolewa na Makamu wa Kwanza wa Rais, yazingatiwe na kufanyiwa kazi kwa kila mmoja kufahamu masuala ya msingi kwa lengo la kuleta ufanisi.

Wakurugenzi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, waliahidi kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo katika kushughulikia masuala yao ya kiutendaji pamoja na kuhakikisha wanasimamia vyema maslahi ya watumishi, kuhudumia wananchi.

# Kunawa mikono sasa jambo endelevu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kupambana na magonjwa ikiwamo corona, shule za msingi, sekondari na masoko ni miongoni mwa maeneo yatakayowekewa miundombinu ya kunawa na jamii kuhamasishwa kusafisha mikono ili kujikinga na maradhi.

Ili kufikia azma hiyo, sehemu nyingine zitakazokuwa na huduma hizo ni masokoni, vituo vya mabasi na ofisi za watendaji kata na serikali za mitaa.

Haya yamebainishwa mwishoni mwa wiki na Mtendaji Mkuu wa asasi ya 'My Legacy,' Fortunata temu, inayokusudia kutoa huduma hiyo katika kata tatu za Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Fortunata akizungumza kwenye mkutano wa kutambulisha mradi huo kwa wadau, alisema kwenye mkutano wa majadiliano kuwa asasi hiyo itaweka miundombinu ya kunawa.

Aliyataja mapipa ya maji, ndoo na sehemu za kuwekea sabuni kuwa vitatolewa wakati jamii (wanufaika) iwe shule, soko, ofisi au kituo cha mabasi watayajaza maji, kuweka sabuni na kuilinda huduma hiyo na kuhamasisha wanufaika kunawa na maji tiririka na sabuni.

"Tunalenga kufikia kaya 2,000 takribani watu 10,000 kwenye kata za Kunduchi, Wazo na Kawe tukiweka vifaa vya kunawa, kuhamasishaji unawaji kama njia nafuu na rahisi ya kujikinga na magonjwa."

Kadhalika, anataja lengo la My Legacy, katika kuitumikia jamii ni kuwafikia wanawake na vijana, kuboresha biashara zao pamoja na makazi ikiwamo sehemu wanazofanyia kazi.

"Tungependa mradi uwe endelevu kwa kuipa jamii jukumu la kuzalisha sabuni kwa gharama nafuu na kwa tija ili zitumike kwenye vituo vya kunawa mikono," anasema Fortunata.

Wakichangia kwenye mkutano huo wajumbe kutoka kata ya Kawe walipendekeza shule zenye wanafunzi wengi ikiwamo Sekondari ya Ukwamani na shule za msingi Kawe A na B ziwekewe huduma hizo.

Aidha kwa upande wa kata za Wazo walipendekeza sekondari ya Kisauke kuingia kwenye mradi kigezo kikiwa ni idadi kubwa ya wanafunzi na ukosefu wa huduma hizo. Aidha, wajumbe waliunga mkono kuweka maji , sabuni na kuhamasisha jamii kunawa mikono kwenye ofisi za watendaji kata na serikali za mitaa kwa vile zinatembelewa na maelfu ya watu kwa siku.

Wajumbe walisema kwa wastani takribani watu 1,000 hufika kwenye ofisi hizo kila siku kuomba huduma, hivyo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni ni suala lisilokwepeka.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Binafsi (Uhuru Banking), Ruth Mwaiselage, kutoka benki ya Stanbic Tanzania, akikabidhi zawadi kwa Meneja Mwandamizi Rasilimali Watu wa TANESCO, Francis Noah Sangunaa, baada ya hitimisho la Mkutano Mkuu wa Mameneja Rasilimali Watu wa TANESCO, ambapo benki hiyo ilitoa elimu ya fedha. **MPIGAPICHA WETU**

# GGML yaanza uchimbaji wa chini kwa chini

**Na mwandishi wetu**

Kampuni ya uchimbaji dhahabu mkoani Geita (GGML) imeanza kuchimbaji wa wazi na wa chini kwa chini katika mgodi wa Nyamulilima ikiwa ni siku chache baada ya Serikali kuidhinisha mpango huo kwa mwaka 2021.

Hatua imekuja baada ya GGML kupokea ruhusa ya mpango wa uchimbaji madini kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Migodi yote nchini, Dk. Abdul Rahman Mwanga.

Dk. Mwanga aliruhusu mpango huo mwishoni mwa wiki baada ya GGML kupeleka nyaraka zote Tume ya Madini na kupatiwa vibali.

Kufuatia ruhusa hiyo, GGML sasa inatarajiwa kufanya shughuli zake za uchimbaji kama zinavyoainishwa kwenye kijitabu kilichokamilika na kutiwa saini na Mkaguzi Mkuu wa migodi yote nchini. GGML inapaswa pia kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia masharti na miongozo ya sheria za nchi ya Tanzania.

Vile vile, Kampuni itaweka taarifa mpya kila mwaka katika mpango wa uchimbaji uliothibitishwa na kwa kuzingatia mabadiliko makubwa katika shughuli za uchimbaji.

Akizungumzia ruhusa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson aliipongeza serikali kwa kuendeleza ushirikiano wa miaka mingi na kufafanua kuwa GGML sasa itapata fursa ya kupanua wigo zaidi wa uzalishaji na kutimiza matarajio ya wadau wake.

"Kupata kibali cha mpango huu wa uchimbaji ni ushahidi wa rekodi yetu nzuri ya uchimbaji madini nchini. Hii inaonyesha pia imani iliyonayo Serikali kwa kampuni yetu kama mdau wa maendeleo," alisema Jordinson.

Miradi inayotajwa katika mpango wa uchimbaji wa GGML ni pamoja na Mradi wa Nyamulilima utakaohusisha maeneo ya kituo cha nane (8), Star and Comet, Xanadu, Selous, Mabe pamoja na Roberts. Uchimbaji wa wazi katika eneo la Nyamulilima unatarajiwa kuongeza uzalishaji dhahabu katika mgodi wa GGML ambapo uchimbaji unaweza kuendelea hadi mwaka 2027.

"Ruhusa ya kuanza shughuli za uchimbaji katika eneo la Nyamulilima ni habari njema kwa wadau wetu, wafanyakazi na wakandarasi. Inatoa pia fursa nyingi kwa jamii inayotuzunguka kufaidika kutokana na shughuli za AngloGold Ashanti. Tunatarajia kuendelea kufanya uwekezaji kwenye jamii inayotuzunguka kwa kuwa hiyo ni mojawapo ya tunu zetu," aliongeza Jordinson.

Naye Kaimu Meneja Mkuu wa GGML Wayne Louw, alisema uzinduzi huo wa uchimbaji katika mgodi wa Nyamulilima umetimiza ahadi ya kampuni hiyo kwa wadau wake wakiwamo wafanyakazi na wakandari.

Hivi karibuni GGML iliibuka mshindi wa jumla wa kampuni zinazofanya vizuri kwenye sekta ya madini nchini Tanzania kwa mwaka 2019/2020. GGML iliibuka mshindi katika vipengele vya Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR), utunzaji mazingira na usalama, ukusanyaji wa mapato ya Serikali (kodi) na uwezeshaji wa wazawa.

# Wanafunzi, wajasiriamali Kibiti wakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Kibiti mkoani Pwani imenufaika kwa msaada wa madawati wa elimu na ujasiriamali.

Imekabidhiwa madawati 250, viti pamoja na meza 250, huku wajasiriamali wanawake wakijengewa uwezo.

Msaada huo umetolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ikiwa ni sehemu ya Mpango wa uwajibikaji wa Jamii ambao unalenga kuchangia utoaji wa elimu bora nchini.

Kadhalika, benki hiyo pia imetoa mafunzo ya kibiashara na ujasiriamali kwa wanawake wajasiriamali 150 wilayani humo ili kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara zao kwa ufanisi, huku wakizingatia nidhamu ya fedha kabla hawajapatiwa mikopo kwa ajili ya kukuza mitaji yao.

Madawati hayo yalikabidhiwa na Mkurugenzi wa Idara ya wateja wadogo wa benki hiyo, Elibariki Masuke, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Gullamhussein Kifu. Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Mbunge wa Kibiti, Twaha Mpembenwe na maofisa wengine wa wilaya hiyo akiwamo mkurugenzi mtendaji.

Masuke alisema benki hiyo imejitolea kusaidia katika kuboresha ustawi wa jamii kupitia misaada ya kijamii ikiwamo elimu, na kwamba wameguswa sana na suala la changamoto ya madawati kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini hivyo kuchukua hatua hiyo kuboresha zaidi sekta hiyo.

Kuhusu mafunzo kwa wajasiriamali wanawake, Masuke alisema miongoni mwa sababu zinazokwamisha utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wengi ni pamoja na wao kuendesha biashara zao bila kuzingatia misingi ya kifedha ikiwamo kutunza kumbukumbu za mahesabu ikiwamo mapato na matumizi.

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Chad lakabiliana na waasi FACT

**Mao,** CHAD

MAKABILIANO ya kwanza kati ya vikosi vya serikali na waasi wa Front for Alternation and Concord in Chad (FACT), yalizuka Kaskazini mwa mji wa Mao, katika Mkoa wa Kanem.

Msururu wa waasi hao, waliovuka mpaka na kuingia kwenye ardhi ya Chad kutoka Libya, Aprili 11, mwaka huu, uliingia katika eneo hilo lililoko chini ya kilomita 300 kutoka mji mkuu kabla ya kukabiliana na vikosi vya serikali.

Mapigano hayo yalifanyika karibu siku ya Jumamosi kaskazini mwa Kanem.

Waasi walioripotiwa siku mbili zilizopita huko Gouri, kilomita 200 Kaskazini mwa mji wa Faya Largeau, walitoweka kutoka kwenye rada na kuonekana tena katika eneo la Kusini.

Jeshi lililopewa taarifa kutoka kikosi cha wanaanga, lilikuwa likisubiri waasi katika eneo hilo, lenye matuta ya mchanga.

Kwa sasa hakuna idadi ya watu waliouawa au kujeruhiwa katika mapigano hayo, ingawa jeshi lilisema limewashinda wale linalowaita magaidi.

Kulingana na vyanzo kadhaa vya usalama, waasi wamegawanyika katika makundi kadhaa kushambulia pande kadhaa, hali ambayo inawafanya waseme kwamba mapigano ya Jumamosi hayawezi kuwa ya mwisho.

Hali hiyo ilitia wasiwasi serikali ya Ndjamena, baadhi ya watu walianza kuweka vyakula vya akiba kwenye ghala zote.

Tovuti ya ubalozi wa Ufaransa nchini Chad, kulichapishwa habari inayowashauri raia kuepuka kutoka mji mkuu. **RFI**

# Mlipuko kiwanda waua China

**Shanxi.** CHINA

WATU wawili wamefariki katika mlipuko kwenye kiwanda cha kemikali Kaskazini mwa China.

Pia watu watatu hawajulikani walipo.

Kulingana na ripoti ya kituo cha televisheni cha China, CGTN, mlipuko ulitokea katika kiwanda hicho kilichopo, Tayyuan, Shanxi.

Mamlaka iliripoti kwamba watu wawili wamepoteza maisha na watatu hawakupatikana katika mlipuko huo.

Jitihada za kutafuta na kuokoa zinaendelea kwenye kiwanda. **TRT**

# DRC kupunguza balozi zake ikikabiliwa tatizo kifedha

**Kinshasa,** DRC

BALOZI za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kote duniani zinakabiliwa na matatizo makubwa ya kiutendaji.

Baadhi ya balozi za nchi hiyo, zinakabiliwa na malimbikizo ya hadi miezi 12 na kodi na mishahara ambayo hailipiwi tena.

Waziri wa Mambo ya Nje, Marie Tumba Nzeza, alisema hayo katika vyombo vya habari akiomba kuhusika zaidi kwa serikali ya DRC ili kumaliza matatizo hayo.

**Kinshasa inataka kubadilisha sera yake ya kigeni kulingana na changamoto za sasa.**

Kwa mujibu wa mwandishi wa RFI, Kinshasa, Patient Ligodi, mchakato wa urekebishaji ulizinduliwa wiki iliyopita, Aprili 12.

Agizo lililotolewa kwa Benki Kuu ya DRC na kati ya kiasi kinachokadiriwa kuwa dola milioni 9.3 zitatolewa, kulingana na vyanzo kutoka Wizara ya Mambo ya nje.

Kipaumbele kitatengwa kwa kodi ili kuhifadhi picha ya nchi, kulingana na ofisi ya rais wa Jamhuri na serikali kuchukua hatua ya kupunguza idadi ya balozi.

Pamoja na matatizo hayo ya kimazingira, serikali inatarajia kuchukua hatua sahihi.

"Kuna haja ya wazi ya kuleta utulivu katika sekta hii," alisema ofisa mwandamizi katika ofisi ya rais.

Nchi hiyo kwa sasa ina balozi karibu 60 duniani.

Mageuzi yaliyotangazwa yanapaswa kujikita katika kupunguzwa kwa idadi hiyo kwa sababu za kibajeti.

Kinshasa inataka kubadilisha sera yake ya kigeni kulingana na changamoto za sasa. **RFI**



Wanawafalme wakisindikiza gari lililobeba jeneza la babu yao, Mwanamfalme Philip (99), aliyefariki dunia Aprili 9, mwaka huu na kuzikwa katika makaburi ya Windsor Castle, Uingereza, juzi. Wakiongozwa na Mwanamfalme Charles, Andrew, Edward, William, Phillips na Harry. **PICHA: AP**

# Vifo corona vyafikia mil. 3 duniani

**Paris,** UFARANSA

IDADI ya watu waliokufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19, imepindukia milioni tatu kufikia mwishoni mwa wiki, licha ya kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa huo ikiendelea kushika kasi.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la habari la Ufaransa, AFP zaidi ya vifo 12,000 duniani kote viliripotiwa kila siku katika muda wa wiki moja iliyopita na kupindukia vifo milioni tatu kufikia Jumamosi.

Pia watu 829,596 waliambukizwa virusi vya corona siku ya Ijumaa pekee, idadi hiyo ikiwa ya juu zaidi kwa watu kuambukizwa kwa siku moja.

Mji mkuu wa India, New Delhi, siku ya Jumamosi ulizifunga shughuli zake za umma baada ya kurekodi visa vipya 234 vya corona pamoja na vifo 1,341.

Ufaransa ilitangaza kuwa nchi hiyo itaweka masharti kwa watu wanaowasili nchini humo kutoka Argentina, Brazil, Chile na Afrika Kusini kukaa karantini ya lazima kwa siku 10 kufuatia wasiwasi wa aina mpya ya kirusi cha corona.

Ndege kutoka mataifa hayo hazitapigwa marufuku, ingawa abiria wanaotokea nchi hizo watatakiwa kukaa karantini la sivyo wakabiliwe na faini.

Ufaransa ilitetea uamuzi wake wa kutopiga mafuruku safari za ndege kutoka mataifa matatu ya Argentina, Chile na Afrika Kusini kwa kusema aina mpya ya kirusi kilichopatikana katika nchi hizo haijafikia kiwango cha kutisha kama kilichoshuhudiwa nchini Brazil.

Hatua hizo mpya za karantini zitaanza kutekelezwa hatua kwa hatua katika siku zijazo hadi zitakapotekelezwa kikamilifu kufikia Jumamosi ijayo.

Hivi karibuni, Ufaransa iliimarisha vikwazo vyake vya kupambana na wimbi la tatu la virusi vya corona.

Uingereza ambayo tayari imetoa chanjo kwa asilimia 60 ya raia wake angalau kwa dozi ya kwanza, sasa inarekodi takriban vifo 30 kwa siku kutoka vifo 1,200 vilivyokuwa vikirekodiwa mwishoni mwa mwezi Januari.

Uhispania iliongeza muda wa karantini ya lazima kwa abiria wanaowasili kutoka katika nchi 12 za Amerika Kusini na Afrika, zikiwamo Brazil na Afrika Kusini.

Siku moja baada ya Italia kutangaza kupunguza sehemu ya hatua zake za kukabiliana na kuenea kwa virusi vya corona katika shule na mikahawa kuanzia Aprili 26, wafanyakazi kwenye tasnia ya burudani waliandamana siku ya Jumamosi mjini Roma wakitaka msaada zaidi wa serikali. **DW**

# GUADIOLA AJITETEA MAN CITY IKITUPWA FA



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema licha ya kufanya mabadiliko kwenye kikosi chake kutoka kile ambacho kilishinda mbele ya Borussia Dortmund kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita, bado alikuwa anawaheshimu wapinzani wake Chelsea kwenye mchezo wake wa nusu fainali ya Kombe la FA.

City juzi ilifungwa na Chelsea bao 1-0 kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA kwa bao la Hakim Ziyech dakika ya 55 na kufanya Blues hao kutinga fainali.

Guardiola mara baada ya mchezo huo alisema:"Unadhani kwamba sikuweza kuweka nguvu kubwa kwenye mchezo wetu wa Kombe la FA?

"Unadhani kwamba Sterling ama Ferran Torres ama Gabriel Jesus hawastahili kucheza mchezo huu.

"Hatukuwa tumekata tamaa tulikuwa tunahitaji kufika kwenye fainali ya Kombe la FA ila tumepoteza. Kwa maana hiyo ikitokea umeshinda ina maanisha kwamba uamuzi ulikuwa mbaya? Timu ambayo imetinga hatua ya nusu fainali huwezi kuibeza labda useme kwamba tumepoteza mchezo hilo lipo wazi.

"Ulikuwa ni mchezo mgumu ninawapongeza wapinzani wetu Chelsea kwa ushindi. Licha ya kuwa na mabadiliko ya wachezaji hawa nane, unadhani kama ingetokea tukashinda hapo mambo yangekuwaje? "

# Norwich Man City yarudi EPL

**LONDON,** England

NORWICH City imerejea Ligi Kuu England ikiwa imetumikia msimu mmoja tu kwenye Ligi Daraja la Kwanza baada ya kushuka msimu uliopita wa 2019-20.

Miamba hao wamethibitisha kurejea kwenye Ligi Kuu England kwa msimu wa 2021-22 baada ya Swansea kushindwa kuifunga Wycombe nyumbani na Brentford kutoka suluhu na Millwall.

Swansea City ilitoka nyuma kwa mabao 2-0 kusawazisha mabao hayo mawili ndani ya dakika tatu, lakini walishindwa kupindua meza na kushinda mechi hiyo, huku Brentford wakishindwa kupata ushindi mbele ya Millwall kwa kutoka sare ya bila ya kufungana, kitu ambacho kilikuwa habari njema kwa Norwich inayonolewa na kocha Mjerumani Daniel Farke.

Norwich ilishuka kutoka Ligi Kuu England msimu uliopita, lakini waliweka matumaini yao kwa kocha huyo Mjerumani na kubaki naye, ambaye kwa sasa amewarudisha kwenye ligi hiyo.

Norwich ilimaliza nafasi ya mwisho kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita, ikiwa imevuna pointi 21 tu, ambapo ilishinda mechi tano tu. Hii ni mara ya nne kwenye kipindi cha miaka 10, Norwach City imekuwa ikishuka na kupanda Ligi Kuu England.





# Silva kuwa mbadala wa Haaland United

**MANCHESTER,** England

WAKATI Manchester United wakiendeleza jitihada zao za kuimarisha kikosi chao hasa eneo la ushambuliaji, jina la Andre Silva limeibuka kama moja ya malengo ya klabu hiyo.

Silva amekuja kama moja ya malengo hayo kutokana na usajili wa Erling Haaland kuonekana kuwa mgumu, baada ya nyota huyo wa Borussia kutaja dau la mshahara mkubwa kwa wiki endapo atasajiliwa klabuni hapo.

Silva anakipiga katika klabu ya Frankfurt, mpaka sasa ana mabao 23 katika michezo 26 aliyocheza ya Bundesliga, akiwa nyuma ya Lewandowski mwenye mabao 35.

Dau lililotajwa kwa Silva ni euro milioni 40, tofauti na Haaland ambaye aliwekewa kiasi cha euro milioni 180 na mshahara mkubwa mno.

Silva anaweza kuwa ingizo muhimu sana endapo tu kocha Ole Gunnar Solskjaer na Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Edi Woodward wataamua kufanya usajili huo.

## HABARI MICHEZO

# ARTETA AMCHIMBA MKWALA PEPE



**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amemuonya nyota wake, Nicolas Pepe, kwamba atamuondoa kwenye kikosi cha kwanza ikiwa ataendelea kuonyesha kiwango cha chini.

Pepe aliyesajiliwa miaka miwili iliyopita akitokea Lille kwa pauni milioni 72, anaonekana kuchelewa sana kuonyesha kiwango kilichotarajiwa wakati anajiunga na 'Washikabunduki' hao.

Hivyo, baada ya kumvumilia kwa muda mrefu, Arteta anaonekana kukwazika na kiwango cha kupanda na kushuka cha mchezaji huyo.

Pepe mwenye umri wa miaka 25, alifunga bao lake la 10 la msimu wakati Arsenal ikifuzu robo fainali kwenye michuano ya Ligi ya Europa dhidi ya Slavia Prague uliomalizika kwa ushindi wa mabao 4-0.

"Wote tunajua kwamba Nico ana uwezo mkubwa wa kufanya vizuri na tupo tayari kumpa ushirikiano ili auonyeshe," alisema Arteta wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Muda huu suala hili linabaki kwake binafsi kwa sababu anahitajika kutuliza akili yake ili kuwa kwenye kiwango tunachotarajia.

"Kiwango alichoonyesha kwenye michezo michache iliyopita hususan ya Europa League ndio nitakwenda kukidai kwenye mechi zinazofuata za michuano yote na kama ataonyesha chini ya hapo hatapata nafasi ya kucheza,

## Koeman: Sasa nataka taji la LaLiga Barcelona



**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman amebainisha kwamba, baada ya kutwaa taji lake la kwanza akiwa kocha wa Barcelona, sasa akili yake inawazia Kombe la Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Barcelona walitwaa Kombe la Mfalme (Copa del Rey) juzi Jumamosi baada ya kushinda kwenye fainali mabao 4-0 dhidi ya Athletic Bilbao, na kuwa taji la kwanza kwa raia huyo wa Uholanzi hapo Camp Nou ambako alichukua mikoba Agosti.

Miamba hao wa Catalunya walipoteza kwenye fainali ya Supercopa kwa Bilbao Januari na walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 na Paris Saint-Germain.

Barca wapo kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi, wakiwa nafasi ya tatu katika msimamo wakipitwa pointi mbili na vinara Atletico Madrid pamoja na Real Madrid.

"Kushinda taji ni muhimu kwa upande wangu," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Licha ya mabadiliko kwenye klabu na wachezaji vijana, Barca itaendelea kupambana ili kubeba mataji zaidi.

Katika fainali hiyo ya Jumamosi, mabao ya Barcelona yalifungwa na Antoine Grizemann, Frenkie de Jong na Lionel Messi aliyefunga mawili.

## *Kane azua tena hofu Spurs*

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, amepata majeraha wakati akiisaidia timu hiyo kupata pointi moja, Ijumaa kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Everton pale Goodison Park.

Kane amepata majeraha hayo ikiwa ni siku sita zimesalia kabla ya mchezo wa fainali ya Carabao Cup ambao watacheza dhidi ya Manchester City.

Alipata majeraha ya enka wakati akiokoa kwa kichwa kona iliyopigwa langoni mwao.

Mara baada ya mchezo huo kumalizika na kwenda sare ya mabao 2-2, kocha wa Spurs, Jose Mourinho alisema, "Sina jibu la moja kwa moja kuhusu majeraha yake, lakini nitaliongelea hilo hivi karibuni kwa sababu sijui kaumia kwa kiasi gani."

Kane alikuwa kwenye kiwango bora katika mchezo dhidi ya Everton, alianza kwa kuitanguliza timu yake dakika 27, bao hilo lilisawazishwa dakika 31 na Gylfi Sigurosson ambaye aliifungia tena Everton bao la pili dakika ya 61 kwa penalti.

Dakika ya 68 aliirudisha mchezoni Spurs kwa kuifungia bao la kusawazisha na mwishowe mchezo huo kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 na timu hizo mbili kugawana pointi.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YATIA MGUU SAINI YA STERLING CITY

●●● Kwa sasa mazungumzo ya mkataba wake mpya hapo Etihad yamesimama na taarifa...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeonyesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Manchester City, Raheem Sterling, kwa mujibu wa Daily Star.

Sterling kwa sasa amepoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza pale Man City na hivyo kuibua uvumi wa kwamba anataka kuondoka ndani ya Klabu hiyo.

Phil Foden amechukua nafasi ya Sterling na amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho, ikiwamo kufunga bao la ushindi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund wiki iliyopita.

**Mazungumzo ya mkataba mpya kwa Sterling yamesimama na uvumi unabainisha kwamba, Man City wenyewe hawajaonyesha nia ya kutaka kumuongezea.**

Mkataba wa sasa wa Sterling na City umebakiwa na misimu miwili na imeripotiwa kwamba, ada yake inaweza kuwa pauni milioni 80 kwa timu yoyote itakayomtaka.

Na sasa Madrid wamejitosa kuwania saini yake wakati wa dirisha la uhamisho la majira ya joto linalokuja.

Sterling alijiunga na Man City akitokea Liverpool mwaka 2015 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 44.

## ZISIKUPITE

### MUORINHO HALI TETE

KUNA uwezekano mkubwa Jose Mourinho hataendelea kuwa kocha wa Tottenham Hotspur msimu judo wakati wakiwa hawana uhakika wa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Football London)***

### POGBA ATAKA MSHAHARA

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba, 28, anataka mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki ili kusaini mkataba mpya na Manchester United, huku Real Madrid, Paris St-Germain na Juventus zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo. ***(Star on Sunday)***

### VARANE AGOMBEWA EPL

CHELSEA itashindana na Manchester United kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa kati wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane, 27. ***(Bild)***

### WOLVES KUMUUZA TRAORE

KLABU ya Wolves inataka kumuuza winga wake, Adama Traore, 25, ili kutafuta fedha za usajili na pauni milioni 30 zinaweza kutosha kumuachia mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### SPURS WAMTAKA EMERSON

KLABU ya Tottenham Hotspur inaendelea kumfuatilia mlinzi wa kulia wa Brazil, Emerson, 22, ambaye anacheza kwa mkopo kule Real Betis akitokea Barcelona. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### WIJNALDUM HUYO BARCA

KIUNGO wa Liverpool, Georginio Wijnaldum, 30, anapanga kujiunga na Barcelona kipindi cha majira ya joto kwa sababu anataka kucheza na Lionel Messi na mchezaji mwenzake wa Uholanzi, Memphis Depay. ***(Sunday Mirror)***

### ABRAHAM NA HATIMA YAKE

MAJALIWA ya straika wa England, Tammy Abraham, pale Chelsea yapo shakani baada ya kocha, Thomas Tuchel, kutoonyesha nia ya kumuweka kikosi cha kwanza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail on Sunday)***

### TOMORI KUSAJILIWA JUMLA

AC Milan imeijulisha Chelsea kwamba inataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu, Fikayo Tomori, mwenye umri wa miaka 23, ambaye anacheza hapo kwa mkopo. ***(Football Insider)***

### LOFTUS-CHEEK AWINDWA

ASTON Villa na Crystal Palace zinawania kumsajili kiungo wa Chelsea na England, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 25, ambaye anacheza kwa mkopo kule Fulham. ***(Teamtalk)***

### LEEDS YAMTAKA TAGLIAFICO

LEEDS United inataka kumsajili mlinzi wa kushoto wa Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake na Ajax unamalizika mwaka 2023. ***(Sunday Mirror)***

# HABARI MICHEZO



Wachezaji wanaounda kikosi cha timu ya Taifa 'Taifa Stars, inayodhaminiwa na SBL. **PICHA: MAKTABA YETU**

## 'Mzimu' wa Baraza waitesa Biashara

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya juzi, Jumamosi kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga, Kaimu Kocha Mkuu wa Biashara United, Marwa Chamberi, amesema kikubwa kinachoisubua timu hiyo ni kukosa tu kujiamini kama ambavyo walijengewa na Kocha Mkuu, Francis Baraza.

Biashara ambayo ipo katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, haijafanya vizuri mechi zote tatu tangu kuondoka kwa Baraza aliyejiunga na Kagera Sugar kipindi cha mapumziko ya mechi za kimataifa na kupisha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Lakini akitoa sababu ya kupoteza mechi ya juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Yanga, Chamberi alisema katika mchezo huo waliingia na mipango ya kukaa nyuma mpira kusubiri wapinzani wao wafanye makosa, ila walipofanya makosa walishindwa kuyatumia kufunga.

"Wachezaji wanapoteza kujiamini kutokana na kupoteza mechi, unapopoteza wazi unapoteza kujiamini, hivyo mchezo ujao ni lazima ufanye juhudi zaidi.

"Hawajiamini kama ambavyo tulivyokuwa na mwalimu wetu [Baraza], ila mashabiki waendelee kutuunga mkono zaidi, ninaimani tutafanya vizuri katika mechi zijazo," alisema.

Biashara United itashuka katika Uwanja wa Uhuru kesho kuivaa KMC FC ambayo nayo imeonyesha kuimarika zaidi kwenye Ligi Kuu ikiwa nafasi ya tano na pointi zake 39 baada ya mechi 26.

# SBL KUENDELEA KUCHANGIA MAENDELEO YA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imesema itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuchangia sekta ya michezo hapa nchini ambayo pia inaajiri Watanzania wengi kupitia shughuli mbalimbali zilizopo ndani ya sekta hiyo.

**Serengeti imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo ya michezo na imekuwa ikifadhili michezo mbalimbali ikiwamo soka, riadha na gofu.**

Mkuu wa kitengo cha Bia wa SBL, Anitha Msangi, aliliambia gazeti hili kuwa kampuni hiyo inatambua mchango wa michezo na kwamba kupitia Chapa ya Serengeti imekuwa mstari wa mbele kuchangia maendeleo katika sekta hiyo.

Ni kupitia chini ya udhamini wa Bia ya Serengeti Lager, timu ya Taifa, Taifa Stars iliweza kufuzu mashindano makubwa kabisa barani Afrika ya Mataifa ya Afrika (AFCON) yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2019, ambapo ilifuzu mashindano hayo ikiwa ni miaka 39 tangu ifuzu kwa mara ya mwisho.

Kabla ya kufuzu mashindano hayo makubwa barani Afrika, SBL kupitia kinywaji chake cha Serengeti Lager ilisaini mkataba wa miaka mitatu na TFF ambapo ilitoa kiasi cha Sh. billion 2.1 kuidhamini Taifa Stars katika kipindi cha miaka mitatu, udhamini ambao ulikuwa na mafanikio makubwa kwa timu hiyo.

Octoba mwaka 2020, Bia ya Serengeti Premium Lager (SPL) iliingia makubaliano na kusaini mkataba na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa ajili ya kuidhamini Taifa Stars kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Rais wa TFF, Wallace Karia, amesema SBL kupitia chapa ya Serengeti imekuwa ni mfano wa kuigwa katika kuchangia maendeleo ya michezo na kuzitaka kampuni nyingine kuiga mfano.

Mkataba huo unaogharibu Sh. bilioni tatu za Kitanzania, umesainiwa baada ya ule wa awali uliosainiwa mwaka 2017, kufikia ukomo huku timu ikijivunia mafanikio mengi katika kipindi cha udhamini.

Akizungumzia huhusu udhamini wa Taifa Stars Anitha alisema: "Tunaamini kuwa kuiunga mkono Taifa Stars siyo tu tunachangia katika maendeleo ya michezo hapa nchini lakini pia kuongeza hamasa kwa mchezo wa mpira wa miguu ambao unapendwa sana na maelfu ya Watanzania."

SBL kupitia Bia ya Serengeti Lite pia imekuwa mdau mkubwa wa soka la wanawake. Mwaka 2018 Serengeti Lite ilitiliana saini TFF ambapo kampuni hiyo ilitoa kiasi cha Sh. milioni 450 kwa ajili ya kudhamini ligi hiyo. Kupitia udhamini huo, Serengeti Lite inakuwa mdhamini wa kwanza kugeukia Ligi Kuu ya Wanawake ambayo umaarufu wake unakuwa kwa kasi.

# *Mtibwa yahitaji maombi kubaki Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka sare ya bao 1-1 juzi, Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro dhidi ya ndugu zao wa Kagera Sugar, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru (pichani), amesema majaliwa ya timu hiyo kubakia Ligi Kuu au kushuka daraja, yapo kwa Mwenyezi Mungu.

Mtibwa Sugar ambayo Jumatano iliyopita ilikutana na kipigo kizito cha mabao 5-0 dhidi ya Simba, ilionekana kama ingeweza kuvuna pointi tatu nyumbani dhidi ya Kagera Sugar, lakini ikalazimishwa sare na kuzidi kujiweka kwenye hali mbaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu.



"Tumetoka sare ya bao 1-1 na Kagera Sugar. Matokeo haya yametuweka njia panda. Tuko kwenye nafasi mbaya na Jumanne tutacheza na Coastal Union mjini Tanga, lakini kwa matokeo haya tumewaweka mashabiki wentu kwenye wakati mgumu sana. Tuko kwenye msitari mwekundu na mechi tisa zimesalia.

"Lakini kwa yote tunamuachia Mwenyezi Mungu ndiye mwenye uamuzi wa yote kama kushuka daraja au kubaki Ligi Kuu, anaweza kuwafanya wachezaji wetu wapate nguvu ya ajabu na kushinda na kusalia," alisema Kifaru kwa unyonge.

Ni matokeo yanayoiweka Mtibwa kwenye nafasi ya 15, ikiwa juu ya timu tatu za chini.

Ina pointi 25 mpaka sasa kwa mechi 25 ambazo imecheza mpaka sasa.

Timu nne kuanzia ya 18 hadi ya 15 zitashuka daraja moja kwa moja baada ta ligi kumalizika, huku mbili kuanzia ya 14 na 13, zitalazimika kucheza mechi za mchujo na timu za Daraja la Kwanza zilizoshika nafasi za pili kwenye Kundi A na B.

Ikumbukwe msimu uliopita, Mtibwa ilinusurika kushuka kwenye mechi ya mwisho ikiichapa Ruvu Shooting mabao 2-1, huku Mbeya City ikirejea baada ya mechi za mchujo.

Michezo

Jumatatu Aprili 19, 2021

Nipashe



Madrid yatia mguu saini ya Sterling UKURASA 22

KIMOJA TU...



Mshambuliaji na Nahodha wa Simba, John Bocco, akiifungia timu yake kwa kichwa bao pekee wakati wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Mwadui FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kambarage, Shinyanga. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA SC YAIHESABIA YANGA MBILI KILELENI

Bocco arejea kumkimbiza Kagere mbio za Kiatu akiikalisha Mwadui Shinyanga huku...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika ya 66 na nahodha John Bocco limeipa Simba ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC jana jioni, kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

**Lilitokana na mpira wa kona uliyopigwa na Bernard Morrison ambao ulipigwa kichwa na Joash Onyango, kabla ya kumaliziwa na Bocco, akiiandikia timu yake bao pekee kwenye mechi ambayo awali ilionekana nyepesi, lakini kadri muda ulivyozidi kwenda mbele ikageuka kuwa ngumu.**

Ni baada ya Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, kuamua kuwatoa Parfect Chikwende na Jonas Mkude na nafasi zao kuchukuliwa na Bocco, pamoja na Morrison.

Wachezaji hao walioingia ndiyo waliosababisha kupatikana kwa bao hilo, Morrison akipiga kona na Bocco kuujaza wavuni na kumfanya sasa kufikisha mabao 10 msimu huu katika Ligi Kuu akiwa nyuma kwa bao moja dhidi ya straika mwenzake, Meddie Kagere anayeongoza kwa utupiaji.

Mbali na kusababisha bao, Morrison kwa kiasi kikubwa alichangia kuifanya Simba kushambulia kwa kasi kwenye lango la Mwadui, tofauti na kipindi cha kwanza.

Dakika ya kwanza tu Simba ilikuwa kwenye nafasi nzuri ya kuandika bao, baada ya Clatous Chama kutanguliziwa mpira, lakini akiwa peke yake na kipa wa Mwadui, Mussa Mbisa, alipiga shuti lililombabatiza kipa huyo na kurejea uwanjani. Simba ilitawala mpira kwa dakika nyingi za mchezo, lakini ilikuwa ikicheza kwa taratibu mno na pasi fupifupi, kitu ambacho hakikuwasumbua sana Mwadui ambao walikuwa wanashambulia kwa kushtukiza.

Dakika ya 37, Rally Bwalya, akiwa hatua chache kutoka langoni, alipata pasi kutoka kwa Meddie Kagere, lakini shuti lake liligonga nguzo ya pembeni na kurejea uwanjani. Bwalya tena dakika ya 44, alipiga shuti bila kulenga lango akiwa kwenye nafasi nzuri alipiga tena shuti na mpira ukatoka pembeni mwa lango la Mwadui.

Shambulizi la hatari zaidi kwa Mwadui lilikuwa kwenye dakika ya 45, baada ya Hashim Mussa kumlamba chenga Joash Onyango, lakini shuti lake lilipaa juu ya lango la Simba.

Kipindi cha pili Simba ilibadilika baada ya kufanya mabadiliko ilishambulia kwa kasi, lakini wachezaji wa Mwadui walirundikana nyuma na kuifanya mechi kuwa ngumu, hata baada ya kupata bao la kuongoza.

Pamoja na kuwa na baadhi ya wachezaji wazoefu kama Uhuru Selemani, Aziz Gilla, Lucian William ambao wote waliwahi kuichezea Simba, lakini walishindwa kufurukuta mbele ya ukuta wa Simba ukiongozwa na Onyango.

Kwa matokeo hayo, Simba inarudi kwenye nafasi ya pili ikiwa imefikisha pointi 52, nyuma ya vinara Yanga ambayo baada ya ushindi wa Jumamosi dhidi ya Biashara United ilifikisha jumla ya pointi 54.

Hata hivyo, pamoja na kuzidiwa pointi mbili na Yanga, Simba ina pungufu ya mechi tatu, ikiwa imecheza mechi 22 na Yanga 25.

Mwadui inabaki mkiani ikiwa na pointi 16.

## Mwambusi afunguka ukuta kisiki Job, Ninja

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Dickson Job na Abdallah Shaibu 'Ninja' kuonyesha muunganiko mzuri katika safu ya ulinzi ya Yanga dhidi ya Biashara United juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mwambusi, amesema siri kubwa ni namna alivyowajengea kujiamini katika mchezo huo.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0, ikiwa ni mara ya kwanza kwa mabeki hao kucheza kwa pamoja na mara ya kwanza kwa Job kuichezea Yanga.

Akizungumzia kiwango cha Job katika mechi hiyo, Mwambusi alisema ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuichezea timu hiyo na alichokifanya ni kumjengea kujiamini na kumpa maelekezo ambayo kwa kushirikiana na Ninja waliyatekeleza kwa zaidi ya asilimia 60.

"Job hajaicheza Yanga, hii ndiyo mechi yake ya kwanza, lakini pia hakuwa na muunganiko na wenzake, ila kikubwa kashika maelekezo kama nilivyomwambia twende uwanjani kacheze mimi nakuamini na kafanye kazi kwa maana ulipotoka tulikuchukua kutokana na kiwango chako, nataka udhihirishe hapa kama unafaa kucheza Yanga," alisema Mwambusi

Kuhusu mabadiliko aliyoyafanya na kutofanya vizuri kwenye mchezo uliopita, Mwambusi alisema ligi ilisimama kwa muda na wachezaji walikuwa kwenye mapumziko, hivyo waliwaambia sasa kazi ndiyo inaanza na kuwataka kupambana.

"Mimi naamini wachezaji wangu wote na kila siku nawaambia kila mtu atapata nafasi kutokana na kiwango atakachoonyesha," alisema.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi ila walishindwa kuzitumia, hivyo sasa wanakwenda kujipanga zaidi kuelekea mechi ijayo, kesho dhidi ya Gwambina FC itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Kikubwa mwisho wa mechi hii ni maandalizi ya mchezo ujao, nawafahamu Gwambina wana wachezaji wazuri wanaweza kufika katika nafasi, tutakwenda kujipanga kutumia nafasi nyingi tunazotengeneza kupata ushindi," alisema Mwambusi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >